
SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

UKURASA 2



## Samia azionya benki matumizi Sh. trilioni moja zilizotolewa BoT


MAISHA
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili
Samaki wa kupaka mlo tosha
MITINDO
Kapelo zinavyopagawisha vijana
KATUNIKA
NYUSI ZINAZOITA Mwanamke anang'arishwa na wanja

UKURASA 9

Jumapili Machi 6, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0580876
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Walichoteta Samia, Mbowe Ikulu usiku

**CCM** yatoa kauli, yapongeza ujasiri kwenda kuzungumza naye...*Endelea ukurasa 2 &3*



Rais Samia Suluhu Hassan, akibonyeza kitufe kufungua Jengo la Makao Makuu ya Benki ya CRDB, katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la Palm Beach, jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Benki hiyo, Dk. Ally Laay na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi. **Picha zaidi Uk. 05. PICHA: IKULU**

UKURASA 2

## Benki zapewa rungu viwanja vya ubalozini

UKURASA WA 7

## KAMA TUMEWEZA DUBAI EXPO, BASI TUANZISHE TANZANIA EXPO

WIKI hii, jina la Tanzania limevuma sana kitaifa na kimataifa kutokana na kushiriki kwa ...

UKURASA WA 17

## KINACHOENDELEA SASA UKRAINE

ZAIDI ya watu milioni tayari wameikimbia Ukraine, huku idadi kubwa wakielekea Poland, kuomba hifadhi kutokana...

## Dk. Mwinyi awahimiza wanawake uchumi bluu

UKURASA 3




RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwa na Mkewe Mama Mariam Mwinyi, baada ya kufungua Kongamano la Wanawake Zanzibar, lililoandaliwa na benki ya TCB, jijini Zanzibar jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo, Edmund Mndolwa (wa nne kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi (kushoto) na viongozi waandamizi wa SMZ. **PICHA: IKULU**

MICHEZO YANGA KAZINI, SIMBA YATISHA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Samia azionya benki matumizi fedha za BoT

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa fursa kwa sekta ya fedha nchini kuchangamkia viwanja vilivyoko kwenye balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali duniani ambavyo vimekaa muda mrefu bila kuendelezwa, ikajenge majengo ya biashara.

Vilevile, ametoa angalizo kwa benki kuhusu matumizi ya ya Sh. trilioni moja zilizotolewa kwao na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kupitia mpango mahususi wa kuwezesha sekta hiyo kupata mikopo yenye riba nafuu.

Fursa hiyo ya kuwekeza kwenye viwanja vya ubalozini aliitangaza jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua jengo la Makao Makuu ya Benki ya CRDB.

"Nikudokeze kipengele kingine cha uwekezaji ambacho mnaweza kukitumia, jana (juzi) tulikuwa na mkutano wa bajeti, tukajadili bajeti yetu lakini tukakuta kwenye Wizara ya Mambo ya Nje (Ushirikiano wa Afrika Mashariki) kuna viwanja vingi vipo nje ya nchi ambavyo ni mali yetu.

"Mali ya balozi zetu lakini kama serikali tunashindwa kuvijenga, naomba tumieni kama fursa ya uwekezaji, nendeni mkajenge majengo kule, mkodishe mfanye biashara ili viwanja vile tusiendelee kunyang'anywa.

"Kwa sababu tunanyang'anywa tunasikitika, tunarudishiwa, tunanyang'anywa tena bado havijengwi, kuna viwanja vina miaka 20, 15 bado havijajengwa, Ninaomba sana ndugu yangu Abdulmajid, mwenyekiti wa wenzio naomba waunganishe waratibu muitumie hii fursa itakavyowezekana," aliagiza.

Rais Samia pia alisema kuwa ili kubeba mzigo huo, serikali kupitia BoT imeanzisha mpango mahususi kuwezesha sekta hiyo kupata mikopo yenye riba nafuu ambapo zimetengwa jumla ya Sh. trilioni moja.

Alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kukopesha benki kwa masharti nafuu ikiwamo riba ya asilimia tatu ili kuongeza ukwasi na uwezo wa kuikopesha sekta binafsi.

Rais Samia alitoa angalizo kuwa fedha hizo kutoka BoT zisiende kulipa madeni au kurekebisha shaka ya mahesabu iliyopo katika vitabu vyao, bali itumike kuwapa sekta binafsi ili waifanyie kazi.

"Trilioni moja siyo fedha ndogo, mtakumbuka fedha za kutoka kwenye ahueni ya UVIKO 19 Sh. trilioni 1.3 zimefanya mambo mengi. Na hii trilioni moja ikafanye kazi kubwa. Sina shaka kiwango hiki kitaleta matokeo makubwa kwa sekta binafsi kwa kampuni na mwananchi mmoja mmoja.

Pia alisema CRDB ina nafasi kubwa ya kutoa fedha katika sekta ya uzalishaji hasa kilimo kwa kuwa ina fedha za Global Fund (Dola milioni 100) na CRDB (Dola milioni 100) na kufanya kuwa na jumla ya dola milioni 200.

"Wito wangu kwa benki katika bajeti ya mwakani serikali tumeweka kipaumbele kikubwa kwenye sekta ya kilimo na tunazungumzia kilimo cha umwagiliaji maji, hili ndilo eneo litakalotupa mapato kwa haraka.

"Ubelgiji wanakula mchele kutoka Tanzania, Falme za Kiarabu tumesaini mkataba wa mboga, ninawaomba mtupie macho kwenye hili," aliagiza.

Rais Samia alisema miradi yote mikubwa ya kimkakati wamepata msukumo wa benki za ndani na za nje na kueleza kuwa serikali itaendelea kufanya kazi nazo.

"Kama tulivyosema kila miradi mikubwa lazima iwe na kipengele cha wafanyabiashara wa ndani kuweza kufanya biashara au kufanya kazi kwenye hiyo miradi na benki ndizo zitakazowezesha wafanyabiashara wa ndani waweze kufanya hiyo kazi na miradi mikubwa inayokuja," alisema.

Rais Samia aliipongeza CRDB kwa kuwa walipakodi wazuri ambapo mwaka jana walilipa serikalini zaidi ya Sh. bilioni 249.2.

# CRDB yamwahidi Samia fedha za miradi mikubwa

**Na Romana Mallya**

BENKI ya CRDB imemhakikishia Rais Samia Suluhu Hassan itashirikiana na benki za ndani na wadau wa nje kuhakikisha miradi mikubwa, ikiwamo iliyotiwa saini hivi karibuni, inapata fedha.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, wakati wa uzinduzi wa jengo jipya la Makao Makuu ya benki hiyo lililoko Palm Beach jijini Dar es Salaam jana.

"CRDB ina wadau wengi nchi zima na duniani ambako tunawezesha miradi mikubwa kupata fedha kirahisi, tulifanya kwa miradi ya SGR (reli ya kisasa) na tutafanya kwa miradi iliyosainiwa hivi karibuni.

"CRDB tupo tayari kuongoza ili kuhakikisha miradi mingi inapata fedha kwa kushirikiana na benki za ndani na wadau wetu wa nje ili miradi ifanyike," aliahidi.

Nsekela alimweleza Rais Samia kuwa CRDB ndiyo benki pekee kwa Tanzania, Afrika Mashariki na Afrika ambayo imepata usaili kupitia shirika la GCM (Climate Fund), wakisailiwa daraja la kati.

"Tulisailiwa mwaka 2019 lakini katika mwaka mmoja tumeandaa programu mahsusi tukaipeleka GCM, ikapitishwa tukaandaa programu ya nchi kwa kushirikiana na wizara yenye dhamana ya mazingira, Wizara ya Kilimo na wadau wa kilimo, tukaipeleka kuomba dola milioni 100. "Novemba mwaka jana tukapata, CRDB itaongeza dola milioni 100, hivyo programu itakuwa na dola milioni 200 sawa na zaidi ya Sh. bilioni 460, programu inalenga kwenye kilimo cha mazao ya chakula," alibainisha.

Nsekela alisema progamu hiyo itakapokuja, walipendekeza iwe na fungu la kuwajengea uwezo wanufaika na kuwe na uhuishaji ambapo dola milioni 10 zimetengwa. "Kutokana na majanga ya kilimo, itatengwa dola milioni 10 kwa ajili ya bima ya mazao na dola milioni 10 kwa ajili ya kupunguza makali ya dhamana," alifafanua. Nsekela alisema mradi mzima utawafikia Watanzania milioni 1.2 na Watanzania milioni 4.9 watafaidika kupitia wanufaika hao, hivyo watahudumia jumla ya Watanzania milioni 6.2.

Alisema kwa miaka mitatu CRDB imefanya vizuri ambapo mwaka 2019 walipata faida ya Sh. bilioni 64, mwaka 2020 ikafikia Sh. bilioni 165 na mwaka 2021 walipata Sh. bilioni 268, ikiwa ni ongezeko la asilimia 62 la faida. Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa kwa miaka miwili CRDB imelipa kodi ya Sh. bilioni 430 na kupitia wakala na matawi walikusanya kodi ya serikali zaidi ya Sh. trilioni 1.9.

"Tumetoa mchango wetu kwa mradi wa SGR Sh. bilioni 240, mradi wa Bwawa la Nyerere tulitoa zaidi ya Sh. bilioni 500, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Terminal III tulitoa Sh. milioni 40, miradi ya REA (mradi wa usambazaji umeme vijijini) Dola milioni 60 kwa ajili ya makandarasi mbalimbali," alifafanua.

Nsekela alisema CRDB ndiyo benki kubwa ambayo imetoa mikopo mingi kuliko zingine ambapo hadi sasa wametoa Sh. trilioni 5.1 kwa wateja na sekta mbalimbali.

"Ajenda yako Rais ndiyo ajenda yetu, tutakuwa popote ulipo ili kuleta maendeleo. Hatua mbalimbali za serikali inazochukua benki yetu imekuwa ikitoa mikopo kwa kuhakikisha inapatikana kirahisi," alisema. Vilevile, alisema wamepunguza riba ya mikopo kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi kutoka asilimia 18 hadi asilimia 13 na wamekuwa wakitoa mikopo na elimu ya kutafuta masoko kwa wajasiriamali.

"Tuna huduma mahusus ya machinga, kwa kushirikiana na machinga wa Dar es Salaam tunaandaa kanzidata, tunawaandaa kidigitali watoke kwenye sekta isiyo rasmi kwenda sekta rasmi, tutakuwa nao bega kwa bega ili wawe wafanyakazi sahihi, tunakushukuru kwa kuandaa mazingira mazuri kwao ya kufanya biashara," alisifu.

**UBUNIFU WA JENGO**

Nsekela alisema jengo hilo lina ofisi za kisasa, vyumba vya kisasa 60, chumba cha mkutano kinachobeba wageni 200 na kuna huduma maalumu kwa wateja wa kati au maalumu kwa ajili ya kutoa ushauri na uwekezaji.

"Kuna sehemu ya digitali, tunafahamu kuna wafanyakazi na wateja wanataka kufanya miamala, wataingia kwenye self service (jihudumie)," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ghorofa ya pili katika jengo hilo ni makumbusho ya sekta ya fedha, ambayo itakuwa sehemu ya mafunzo ya wataalamu na kwa vyuo vya fedha kupeleka wanafunzi wake kujifunza.



Msomaji maarufu wa Quran Duniani kutoka nchini Marekani, Dk. Hassan Saleh (kushoto), akikabidhi mfano wa nyumba kwa Abdulimalik Sulyman, baada ya kuibuka mshindi wa kwanza wa fainali ya mchujo wa kitaifa kutafuta mwakilishi wa Tanzania, atakayeshiriki kuwania tuzo ya Kimataifa ya kusoma na kuhifadhi Quran Tukufu, katika mchujo uliofanyika Chamazi, jijini Dar es Salaam jana. Wa (pili kushoto) ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Jumuiya ya Kuhifadhi Quran Tukufu Tanzania, Shehe Othuman Kaporo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CCM yatoa kauli Mbowe kwenda Ikulu

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimempongeza Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kwa kile kilichokiita kuonyesha uungwana na kuahidi kumpa ushirikiano Rais Samia Suluhu Hassan kwa ustawi wa Tanzania.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ndiye aliyetoa pongezi hizo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa jengo la Makao Makuu ya Benki ya CRDB.

Alisema CCM imepokea kwa faraja hali ya ustawi wa demokrasia nchini.

"Ninashukuru Freeman Mbowe kwa kuonyesha uungwana kwa sababu amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujali na amemwahidi kumpa ushirikiano kwa ustawi wa Tanzania. Hiyo ndiyo siasa safi, hiyo ndiyo Tanzania tunayojivunia," alisema

Shaka alisema kuwa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025 waliahidi kwenye ibara ya 118 watasimamia ustawi wa demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora.

Alisema serikali imeishi vizuri maelekezo ya ilani kwa kuwa moja ya mambo makubwa iliyozingatia ni suala la utawala bora.

"Siasa safi inahusisha uzalendo, utu, heshima na kuweka mbele maslahi ya taifa kuliko chochote. Rais Samia ni kielelezo katika hili na ameendelea kuthibitisha dhamira yake ya kuijenga Tanzania moja yenye ustawi kwa wananchi wote, tumpe ushirikiano," alisema.

Shaka alisema CCM inawahakikishia Watanzania kuwa itaendelea kuisimamia serikali izidi kuimarisha uhuru wa maoni, misingi ya haki na demokrasia ili kujenga taifa lenye upendo, umoja, amani na mshikamano wakati wote.

"Lengo la CCM katika kipindi hiki ni kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kupata haki kwa mtu mmoja mmoja na makundi mbalimbali. Tunampongeza Rais Samia kwa kuendelea kutekeleza maelekezo haya ya ilani kikamilifu. Hakika kazi inaendelea vyema," alisifu.




Rais wa Rotary Klabu ya Dar es Salaam (RCD), Sati Badhvi (wa tatu kushoto), pamoja na Mkurugenzi wa Miradi, Nikki Aggarwal (wa pili kushoto) na Mwana Rotariani Hamza Kassongo (kushoto), wakikabidhi msaada wa moja kati ya madawati 117 kwa Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (wa pili kulia), kwa ajili ya kusadia shule ya msingi Bunge, jijini humo jana. Wengine ni Ofisa Elimu wa Taaluma wa Jiji la Dar es Salaam, Bertha Mayeka (kulia) na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Leonida Mulekuzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walichoteta Samia, Mbowe Ikulu usiku

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekutana na kufanya mazungumzo usiku na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) saa chache baada ya kiongozi huyo wa upinzani kufutiwa kesi ya ugaidi iliyokuwa inamkabili.

Wawili hao walikutana baada ya Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kumwachia huru Mbowe na wenzake watatu kutokana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha hati mahakamani kuwa haina nia ya kuendelea na kesi hiyo.

Baada ya mawili hao kukutana kwa mazungumzo Ikulu jijini Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana, Rais Samia aliweka wazi sehemu ya waliyoyazungumza, akisema:

"Ndugu yetu, Mheshimiwa Mbowe leo yupo huru, ameachiwa. Kutokana na hilo, nikaona kuna umuhimu wa kukutana naye leo ili tuzungumze mawili matatu.

"Kubwa tulilozungumza kwamba Tanzania hii ni yetu sote, tunatakiwa kushirikiana kujenga Tanzania na katika hilo muhimu ni kujenga kuaminiana kwa misingi ya haki.

"Na tunaposimamia misingi hiyo, kuaminiana, haki na kuheshimiana ndiyo tutapata fursa nzuri ya kuendesha nchi yetu na kuleta maendeleo."

Mbowe alimshukuru Rais Samia kwa kitendo chake cha kuridhia kukutana, akisema: "Nimeona ni jambo la msingi kuja kumwona Mheshimiwa Rais baada ya kuwa magerezani kwa kipindi cha takribani miezi minane, mazungumzo yetu kwanza nimemshukuru Rais kwa kujali.

"Pili, tumezungumza mambo mbalimbali ambayo kwa muda mrefu yamedumaza uhusiano mwema miongoni mwa chama kikuu kinachoongoza taifa letu (CCM) na chama kikuu cha upinzani (CHADEMA).

"Kama alivyozungumza Mheshimiwa Rais, tumekubaliana msingi mkubwa wa kujenga taifa letu katika maridhiano na umoja unaokubalika ni kusimama katika misingi ya haki na pale neno haki linapotawala, amani inakuwapo."

Mbowe alisema wamekubaliana kuijenga haki katika taifa na kila jambo lililopo, Bunge, taasisi za umma na vyama vya siasa vihubiri haki.

"Tukihubiri haki, amani haitakuwa na tatizo. Ili kufikia misingi hii, kuna umuhimu wa kuaminiana, tumekuwa na urafiki wa mashaka kwa muda mrefu na viongozi wa vyama vyetu vikubwa viwili," alisema.

Mbowe alisema wamekuwa wakipitia madhila mengi ambayo hawahitaji kuyataka kwa sababu wanataka watoke hapo waende mbele wafanye siasa za kistaarabu, kuaminiana na kuisaidia serikali itekeleze majukumu yake.

"Serikali nayo inatakiwa kuhakikisha na sisi tunafanya majukumu yetu vizuri, demokrasia itamalaki katika nchi yetu, pawe na furaha ambayo mama (Rais Samia) tayari ameanza kuijenga. Tumempa mama uhakika na yeye ametuhakikishia hayo yatafanyika.

"Tupo tayari kumpa ushirikiano na tunaomba ushirikiano kwa Watanzania wote, watupe ushirikiano na wampe mama ushirikiano tuijenge nchi. Tunataka mama na serikali yake wasaidie kupata maendeleo yetu," alisema.

Mbowe amekaa mahabusu gerezani kwa siku 221 tangu Julai 26 mwaka jana alipounganishwa na washtakiwa wenzake.

# Bil. 249/- zaokolewa matibabu ughaibuni

**Na Faustine Shija**

SERIKALI imeokoa Sh. bilioni 249 zilizokuwa zitumike kugharamia matibabu ya wagonjwa nje ya nchi kuanzia mwaka 2015 lakini sasa matibabu hayo yanafanyika nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo jana jijini hapa, akisema kuwa kabla ya kuboreshwa kwa huduma za kibingwa nchini, wagonjwa 58,000 walipata rufani kwenda nchi za nje kwa ajili ya matibabu na kugharimu Sh. bilioni 374.

Alisema wagonjwa wanatibiwa hapa nchini ambapo serikali inatumia Sh. bilioni 125.3 na hivyo kuokoa Sh. bilioni 249.

"Unafuu huo umetokana na uboreshaji mkubwa wa miundombinu katika hospitali za rufani na hospitali maalumu uliofanywa na serikali na madaktari bingwa kila hospitali za rufani na zile za kanda," alisema Prof. Makubi.

Alizitaja hospitali hizo zilizoboreshwa kuwa ni Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Kibong'oto, Milembe na zile za kanda za Mbeya, Benjamin Mkapa Dodoma, KCMC, Bugando, Hospitali ya Chato na ya mkoani Mtwara.

Akizungumzia hali ya utoaji chanjo ya UVIKO-19 inayoendelea nchini, Prof. Makubi alisema kuwa zaidi ya watu milioni mbili wamechanja na uhamasishaji unaendelea kufanyika kuanzia ngazi ya jamii na mwitikio kwa sasa ni mkubwa kulinganisha na awali.

"Kwenye suala la chanjo kuna maendeleo mazuri, watu wanazidi kuelimika juu ya kupata chanjo hii, na tunategemea idadi ya waliochanja itaendelea kuongezeka," alisema Prof. Makubi.

Aliongeza kuwa utoaji chanjo siyo wa kulazimishana, bali elimu itolewe kwenye mitaa ili kila mwananchi aelewe na akubali kwa hiari yake kuchanja.

Prof. Makubi pia ametoa wito kwa watu wote ambao walichoma chanjo ambazo zinahitaji dozi mbili, kwenda kuchoma dozi ya pili kwa kuwa ili chanjo ikamilike lazima dozi imalizike.

# Dk. Hussein Mwinyi ahimiza wanawake uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wanawake kuchangamkia fursa za uchumi wa bluu badala ya kuwaachia wanaume pekee.

Amesema wanawake wanahitaji elimu jinsi ya kuitumia fursa hiyo kwa sababu baadhi wanadhani kwamba kwa kuwa inahusisha matumizi ya rasilimali za bahari, basi ni suala la wanaume tu.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano la wanawake kuhusu nafasi ya mwanamke katika kukuza uchumi wa bluu lililoandaliwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) lililofanyika mjini Zanzibar .

Alisema uchumi wa bluu umejumuisha uvuvi, utalii, usafiri wa baharini, ujenzi wa bandari za kisasa, kilimo cha mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi na matumizi mengine ya rasilimali za bahari kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira.

Kutokana na hali hiyo, alisema hataki kuona mjasiriamali anakosa mikopo kwa kukosa wadhamini au riba kubwa na tayari serikali imeielekeza Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar kufanya mazungumzo na TCB ili wajasiriamali, hasa wanawake, wasipate usumbufu.

Alisema mwitikio wa taasisi za fedha katika kuendeleza uchumi wa bluu unampa matumaini makubwa ya kufanikiwa katika utekelezaji wa mipango na mikakati iliyopo katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, malengo ya serikali ya kuendeleza uchumi wa bluu yamezingatia mahitaji ya jinsia zote wanawake na wanaume.

Alisema kwa uvuvi, serikali itaendelea kutafuta njia bora ili sekta hiyo kuyashirikisha na kuyanufaisha makundi mengi zaidi ya wanawake.

"Jambo hili linawezekana kwa kutambua kwamba katika miaka ya karibuni uvuvi wa dagaa umekua na faida na tija kubwa zaidi kwa makundi ya wanawake na inasaidia sana katika kukuza ajira," alisema.

Dk. Mwinyi alisema serikali inathamini juhudi za wanawake katika kuendeleza zao la mwani ambalo ni sehemu ya uchumi wa bluu.

Kongamano hilo, alisema lina mipango na mikakati ya kuliendeleza zao hilo kwa kuhimiza matumizi ya mbegu bora pamoja na mbinu za kuliongezea thamani na utafutaji wa masoko. Pia alisema serikali inaendelea na jitihada za kuwapatia mitaji, vifaa na masoko wazalishaji wa mwani.

"Serikali imeweka mkazo maalum wa kuyapatia mikopo makundi mbalimbali ya wanawake wanaojishughukisha na uzalishaji mwani na shughuli zingine za biashara "alisema.

Pia alisema kuna fursa nyingi katika sekta ya utalii ambazo wananchi hawajazitumia vizuri kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha na elimu na kwamba bado bidhaa nyingi zinazohitajika katika sekta ya utalii zinaingizwa kutoka nje ya nchi ingawa zingeweza kutengenezwa Zanzibar ikiwa wajasiriamali watawezeshwa vizuri.

Alizitaka taasisi za kibenki ziendelee kushirikiana na wajasiriamali kwa kuwapatia mikopo yenye unafuu wa riba na kuendelea kuzisogeza huduma za fedha karibu na maeneo yao ya kazi.

Rais alisema uamuzi wa serikali ya Tanzania kuziunganisha benki ndogo zilizokuwepo awali na kuunda benki ya TCB ulikuwa na nia ya kuyanufaisha makundi mbalimbali ya wafanyabiashara, wawekezaji, wajasiriamali na wananchi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TCB, Dk. Edmund Mndolwa, alimpongeza Rais Mwinyi kwa maono mapya ya kuibadilisha Zanzibar kiuchumi. Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alisema TCB imeshatoa mikopo ya Sh. bilioni 127 kwa wanawake na ni walipaji wazuri katika kurejesha mikopo.

MAKALA MAALUM

## KUELEKEA MWAKA MMOJA SAMIA IKULU

# Viongozi wanawake waanika walivyoguswa na Rais Samia

**Na Romana Mallya**

ZIKIWA zimebaki siku 13 kutimia mwaka mmoja kamili tangu Rais Samia Suluhu Hassan aapishwe kushika madaraka hayo, viongozi wanawake wameeleza namna walivyoguswa na utendaji wake.

Viongozi hao walibainisha hayo wakati wa mkutano wenye mada 'Wanawake na Uongozi; Kuelekea Mwaka Mmoja wa Rais Samia Madarakani' uliofanyika jana jioni kwa njia ya mtandao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Dk. Pindi Chana, alisema wanapozungumzia 'Mwezi wa Malkia wa Nguvu na mlingano wa majukumu, wanaona dhamira ya dhati ya Rais Samia kuanzisha wizara hiyo na ile inayoshughulikia Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto.

"Tukumbuke zipo nchi hawana wizara za maendeleo ya jamii, lakini sisi dhamira ya mlingano wa majukumu, wizara ipo na ina bajeti yake na sasa hivi ameongeza, akasema badala ya kuchanganya na afya tutakuwa na waziri maalumu wa afya na maalumu wa maendeleo ya jamii. Hii inaleta dhamira ya dhati," alisema.

Waziri huyo alisema serikali imeboresha maeneo mengi ambapo sekta ya elimu, madarasa yamejengwa kuanzia shule za awali hadi sekondari.

Alisema wanapopata elimu maana yake wanaweza kujiajiri na kuajiri sekta rasmi na isiyo rasmi na kwa sekta ya maji, Rais alisisitiza lazima mama atuliwe ndoo kichwani.

"Miradi ya TASAF fedha zinakwenda, kiuchumi Rais amesisitiza vijana wanawake na makundi yenye ulemavu halmashauri zihakikishe zinatoa asilimia 10 ya mapato kupewa mikopo," alisema.

Waziri huyo alisema uteuzi wa nafasi mbalimbali za serikali na za kisiasa umefanywa na Rais Samia kwa ustadi mkubwa huku sera zikiboreshwa, akitolea mfano mtoto wa kike anayepata ujauzito, sasa anapewa nafasi ya kurejea shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

"Uwezeshaji wa kiuchumi na uwekezaji kutoka nje, hivi karibuni tuliona Rais amekwenda nchi mbalimbali, milango imefunguka tukianzia Jumuiya ya Afrika Mashariki biashara imeongezeka, Dubai Expo, mikataba isiyopungua 30 tumesaini na wawekezaji mbalimbali," alisema.

Alikumbusha kuwa Rais Samia aliteuliwa kuwa kinara kati ya nchi 16 zinazotekeleza moja ya maeneo maalumu sita ambapo Tanzania imefanya vizuri katika uwezeshaji wanawake kiuchumi na usawa wa kijinsia. "Mheshimiwa Rais kupitia fedha alizopata za IMF Sh. trilioni 1.3, alichagua eneo zuri kuzitumia kwa sababu sasa tuna uhakika kwa watoto wa kike na wa kiume kupata elimu. Eneo lingine ni la upatikanaji wa maji na la tatu ni upatikanaji wa umeme wa uhakika na nafuu," alisifu.

Akizungumzia safari nchi iliko-toka, Rais mstaafu wa Bunge la Afrika, Getrude Mongella, alisema wametoka mbali na wengi hawajui namna uhuru ulivyopiganiwa.

"Tumetoka kwenye umaskini wa mama ambao haueleweki, mama alibeba mtoto mgongoni na kipande cha kaniki tu hadi mtoto anakua. Huko nyuma waliolima pamba na kahawa walikuwa ni wanawake.

"Tulikuwa tunajiuliza 'lini tutaona uongozi wa mwanamke tuone uwezo wake?' Mungu alivyo wa ajabu akamchukua Magufuli kutupa adhabu, nadhani alimchukua kutuonyesha kwamba nchi hii kwa mara ya kwanza itaweza kuvunja mwiko kuwa mwanamke anao uwezo wa kuongoza.

"Tuendelee kuuvunja mwiko huu, akija mgombea mwanamke tunauvunja, akija mwanamume tunauvunja," alisema.

Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Elsie Kanza, alieleza namba raia wa Marekani wanavyojifunza kupitia Tanzania, akisema nchi hiyo ni miongoni mwa zinazopigania haki za wanawake na usawa wa kijinsia lakini haijawahi kuwa na Rais mwanamke.

"Tanzania ina mwanamke pekee ambaye ni mkuu wa serikali barani Afrika, hata Makamu wa Rais Marekani wamempata mwaka 2020, miaka mitano baada ya Tanzania kuwa na Makamu wa Rais mwaka 2015, hivyo Wamarekani wanalo la kujifunza kutoka kwetu, hasa suala la uongozi na usawa wa kijinsia," alisema.

Balozi huyo alisema wanawake Watanzania wanapaswa kujifunza kwa wenzao wa Marekani hasa kwenye suala la uvumbuzi wa kisayansi.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, alisema kuwa tangu Rais Samia ashike nafasi hiyo, yapo mambo mengi ambayo ameyafanya ya kimaendeleo ya kimapinduzi. "Umeona amefanya kazi bila kuchoka, amefanya yaliyoachwa na serikali zilizopita na ameanzisha mengine, mwenyewe anajihamasisha katika kutekeleza majukumu yake, anatuhamamisha kuwa hakuna jambo ambalo mwanamke hawezi kufanya.

"Kama ni kujiamini ametupa ya kupitiliza, ameingia madarakani katika kipindi chenye changamoto kubwa na tusingekuwa na msingi mzuri, mfumo mzuri, taasisi ambazo zipo hai kutoka kwa Rais aliyekuwa madarakani, amepoteza maisha na kuingia Rais mwingine.

"Pengine kwa nchi nyingine hususan nchi za kusini mwa Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara, pengine zingeweza kutetereka. Wengi walikuwa na hofu kubwa lakini alituvusha salama.

"Alifanya kwa haiba ya mama, mara nyingi wanawake wanapoingia kwenye uongozi tunatamani kufanana haiba yetu kama wanaume lakini amekaa kwenye haiba yake kama mama, ameunganisha taifa na ametuvusha salama.

"Kuwa na kiongozi aliyetuvusha kipindi kigumu na amefanya mengi. Uongozi wake ni hamasa tosha na kuelekea 2025 wanawake wengi watajitokeza kugombea," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, alitaja mambo matatu aliyojifunza kupitia uongozi wa Rais Samia kuwa ni uvumilivu na utulivu, namna ya kukabiliana na presha ndani na nje ya taasisi na ujasiri wa kuiongoza taasisi kubwa inayohusu maisha ya watu.

Mwanamitindo na Mkurugenzi wa Taasisi ya Flaviana Matata, Flaviana Matata, alisema kuwa akiwa kijana ambaye yupo kwenye biashara, amejifunza mambo matatu kwa Rais Samia ambayo ni pamoja na uongozi shirikishi kwamba ameshikirisha makundi, jinsia na rika mbalimbali katika kufanikisha malengo aliyojiwekea.

Jambo la pili alitaja ni utu na utulivu, akifafanua kuwa Rais Samia aliingia katika wadhifa huo kwa njia ambayo haijazoeleka lakini ipo kikatiba.

"Wengi tulikuwa na woga taifa litaelekea wapi hususani wafanyabiashara, lakini ametuvusha salama kwa maana ya utu na utulivu. Alisafiri na akakutana na kiongozi wa upinzani, Tundu Lissu (Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA), huu ni utu, binafsi sifurahiswi na hali ya Bunge ilivyo sasa lakini ninaamini uchaguzi ujao kutakuwa na mabadiliko.

"Jambo la tatu ni ujasiri, anaongoza nchi ambayo bado ipo kwenye mizizi ya kihistoria ya mfumo dume, ninaamini anajaribiwa kama mwanamke, aliwahi kusema 'mimi ni Rais wa Tanzania na nina jinsia ya kike'

"Anatufundisha kwamba mbali na matatizo mengi tunayopitia kama wanawake kwenye nafasi mbalimbali za uongozi, tusijione ni wahanga kwamba ninaonekana kwa sababu ni wanamke. Tubebe matatizo na kuonyesha ni kiongozi kama wengine na jinsia siyo kigezo," alisema.

Mkutano huo ulidhaminiwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Mtandao wa Mawasiliano ya Simu wa Airtel Tanzania.

Rais Samia aliapishwa kushika wadhifa huo mkubwa zaidi nchini Machi 19, mwaka jana kutokana na kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli kilichotangazwa usiku wa Machi 17, mwaka jana.



Rais Samia Suluhu Hassan, siku alipoapishwa kuongoza nchi.

**HABARI PICHANI**

# RAIS SAMIA AZINDUA JENGO LA MAKAO MAKUU CRDB



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, na viongozi wengine wakuu wa benki hiyo pamoja na serikali, akivuta kitambaa kuashiria ufunguzi wa jengo la makao makuu ya CRDB, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la Palm Beach, jijini Dar es Salaam jana.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela,



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na viongozi mbalimbali wa CRDB, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (wa pili kulia), Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Prof. Florens Luoga (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, baada ya kuzungumza nao.




Sehemu ya wageni waalikwa katika hafla hiyo.

**PICHA ZOTE: IKULU**




Rais Samia akizungumza na viongozi mbalimbali pamoja na wafanyakazi wa CRDB, baada ya kuzindua jengo hilo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hatua ya Rais Samia, Mbowe kukutana ni ukomavu kisiasa

**RAIS** Samia Suluhu Hassan juzi usiku, alikutana na kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, Ikulu, Dar es Salaam ikiwa ni saa chache baada ya kiongozi huyo wa upinzani kufutiwa kesi ya ugaidi iliyokuwa ikimkabili katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Dar es Salaam.

Mbowe na wenzake watatu, walifutiwa mashtaka ya ugaidi yaliyokuwa yakiwakabili baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuiambia mahakama kuwa haina nia ya kuendelea na kesi hiyo ambayo ilikuwa na mvuto wa aina yake takribani duniani kote.

Baada ya mazungumzo ya wawili hao ambao ni viongozi wakuu wa vyama vikuu nchini- Samia kwa upande wa CCM na Mbowe kwa upande wa CHADEMA, walipata nafasi ya kuzungumza kila mmoja na kuweka bayana kile walichokiteta faragha. Rais Samia ndiye aliyefungua pazia kwa kuweka bayana kwamba Mbowe yuko huru baada ya kuachiwa, hivyo akaona kuna umuhimu wa kukutana naye ili watete mawili matatu.

Katika kuvunja ukimya huo, Rais Samia alisema kubwa walilozungumza ni kuhusu Tanzania kwamba ni ya wote, hivyo ni muhimu kujenga kuaminiana na misingi ya haki hatua ambayo itatoa fursa nzuri ya kuendesha nchi na kuleta mafanikio.

Mbowe kwa upande wake, alibainisha kwamba wamezungumza mambo ambayo ni ya kujenga kwa mustakabali wa nchi na kwamba wanatakiwa kushirikiana ili kuijenga Tanzania huku jambo la muhimu likiwa kuaminiana kwa misingi ya haki huku akisisitiza kwamba kuaminiana, haki na kuheshimiana vitawezesha kupatikana kwa fursa nzuri ya kuendesha nchi yetu na kuleta maendeleo.

Sambamba na hilo, Mbowe alisema katika kikao hicho walizungumza mambo mbalimbali ambayo kwa muda mrefu yamedumaza uhusiano mwema baina ya CCM na CHADEMA na kujenga taifa katika maridhiano na umoja unaokubalika ambao ndio msingi mkubwa wa kulijenga taifa katika misingi ya haki, jambo ambalo litazaa amani katika jamii na taifa kwa ujumla.

Kukutana kwa viongozi hao wakuu katika vyama vya siasa nchini, kumefungua ukurasa mpya wa siasa za Tanzania kwa sababu inadhihirisha wazi kwamba ahadi alizotoa Rais muda mfupi baada ya kushika hatamu ya kuongoza nchi zinaonekana kutimia.


Ni mambo mengi yametokea katika miaka ya karibuni ambayo yamesababisha kuonekana kama kuna uhasama baina ya serikali ya CCM kwa upande mmoja na upinzani kwa upande mwingine. Lakini Rais Samia alipoingia madarakani alionyesha dhamira kwamba ana nia ya kuyafuta yaliyopita ili Watanzania waishi kama ndugu bila kujali tofauti zao za kiitikadi na kiimani.

Jambo hilo lilionekana kama limepotea kabla ya kesi iliyofutwa juzi licha ya makundi mbalimbali kuweka bayana kwamba bado kuna mpasuko kama taifa kutokana na mambo yanayoendelea huku baadhi wakiwamo viongozi wa dini wakimwomba Rais atumie busara kumaliza tofauti hizo ambazo hazina mustakabali mwema kwa taifa.

Hata hivyo, hatua ya Rais na Mbowe kukutana imerejesha imani kwa wapenda amani na maendeleo kwamba sasa Tanzania inarejea katika umoja, amani, mshikamano na upendo vitu ambavyo ni muhimu katika ujenzi wa taifa katika kujenga haki na kuaminiana.

Kauli za viongozi hao baada ya kukutana na kuteta mambo kadhaa Ikulu, zimeonyesha kwamba kuna matumaini makubwa ya kujenga maridhiano na kuwa na taifa ambalo linaheshimu misingi ya haki, demokrasia na uhuru bila kwenda kinyume cha misingi ya sheria na Katiba ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



### Siku ya Wanawake Duniani iimarishe usawa wa kijinsia

Na Sabato Kasika

**MACHI 8**, mwaka huu, kitakuwa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ikiwa na kaulimbiu isemayo; 'Kizazi cha Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu; Tujitokeze Kuhesabiwa'.

Wanawake wanaadhimisha siku hiyo, huku kilio chao cha muda mrefu kikiwa ni kutaka usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali kuanzia nafasi za uongozi za kuchaguliwa na kuteuliwa, ili idadi yao iwe sawa na ya wanaume.

Kama ambavyo wamekuwa wakijitanabahisha, hudai kuwa wao ni wengi kuliko wanaume na ni wapigakura wakuu ambao wana uwezo wa kumpa ushindi mgombea kutokana na wingi wao. Pamoja na wingi wao huo, bado kumekuwapo na malalamiko kwamba katika mgawanyo wa madaraka, hawajafikia 50 kwa 50 kwa maana ya idadi sawa kati yao na wanaume.

Hata hivyo, kumekuwapo na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha usawa huo unafikiwa, kutokana na ukweli kwamba, idadi yao katika uongozi unazidi kuongezeka.

Hivyo wanapoadhimisha siku yao hiyo, ni vyema waitumie kwa kuzidi kuimarisha usawa wa kijinsia hasa kwa kuunganisha nguvu zao na kuendelea kudai kile ambacho wanaona hakijatekelezwa. Nasema hivyo kwa sababu katika baadhi ya mikutano yao, huwa wanalalamikiana kuwa bado hawajawa wamoja, na kwamba hali hiyo inasababisha juhudi zao za kudai usawa wa kijinsia kuendelea kusuasua.

Kama tatizo hilo lipo, basi ni vyema wangeliona na kulifanyia kazi, kwani kwa wingi wao wakiamua kuungana, ni wazi wanaweza kuwabwaga wanaume katika nafasi za kuchaguliwa zikiwamo za udiwani, ubunge na hata urais.

Mtindo wa kuendelea kutoungana unaweza kuchelewesha kutimiza ndoto yao ya kutaka usawa wa kujinsia, kwani njia mojawapo inayoweza kuwasaidia kufikia wanachokihitaji, ni kutobaguana kwa itikadi za vyama.

Badala yake waangalie sifa na vigezo na kumchagua mwanamke mwenzao ambaye wanaona anafaa, kwani kigezo kikiwa ni itikadi ya chama, mfumo huo unaweza kuchukua muda mrefu kuwafanya wafikie asilimia 50 kwa 50 katika uongozi, kwani wajanja watatumia udhaifu huo kuendelea kuwabwaga.

Hivyo wanapoadhimisha siku yao, ni vyema kukumbushana kuwa ni muhimu wazibe mianya yote inayoweza kusababisha wabaguane, ili hatimaye wawe kitu kimoja na watimize ndoto yao ya kudai usawa wa kijinsia.

Kwa ujumla ni kwamba utengano ni udhaifu na unaweza kutumiwa kuendelea kuwafanya wawe chini, hivyo ni vyema wanawake wakajiongeza, ili kumaliza kasoro ndogondogo zinazoweza kukwamisha umoja wao. Wanawake wanaweza kuwa chachu ya kuziba pengo la usawa wa kijinsia kwa kuachana na ubaguzi miongoni mwao, ili anapojitokeza mmojawapo kuwania uongozi, basi wamchague bila kujali chama anachotoka.

Kutokuwapo kwa usawa wa kijinsia na ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana huwa kunatajwa kama ukatili wa kijinsia, ambao unapaswa kushughulikiwa ndani ya wanawake wenyewe na hata nje.

Ushirikishwaji wa wanawake katika nafasi mbalimbali huwa unatajwa kama jambo muhimu kwa ajili ya kuhakikisha utulivu, kusaidia kuzuia migogoro na kuchagiza maendeleo endelevu na maendeleo jumuishi.

Katika karne ya 21 vuguvugu la haki za wanawake limeshika kasi na kuwafanya baadhi ya wanawake kushika nafasi mbalimbali serikalini na hata katika mashirika na kampuni ingawa bado kuna haja ya kasi hiyo kuwa kubwa.

Ninaamini kwamba ukubwa au kasi, unaweza kutegemea jinsi wenyewe wanavyoimarisha umoja wao bila kubaguana kwa itikadi za vyama kama ambavyo imekuwa ikitokea, kwa baadhi yao.

Wanapobaguana, maana yake ni kwamba, wanaweka utengano, ambao kwa ujumla unasababisha udhaifu, wanapotafuta usawa wa kijinsia, kwani wanashindwa kutokana na kwamba si wamoja. Usawa wa kijinsia kimsingi ni suala la utawala hasa kutokana na ukweli kwamba dunia imetawaliwa na mfumo dume yenye utamaduni unaodhibitiwa na wanaume na imekuwa hivyo kwa karne nyingi.

Mfumo huo ulianzishwa kuhusu urithi kupitia wanaume na hadi sasa unaendelea kuathiri kila nyanja ya maisha na unachangia kukandamiza baadhi ya watu kuanzia kisiasa, kiuchumi na kwingineko.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Kama tumeweza Dubai Expo, basi tuanzishe Tanzania Expo



Na Pascal Mayalla

WIKI hii, jina la Tanzania limevuma sana kitaifa na kimataifa kutokana na kushiriki kwa kishindo Maonyesho ya 13 ya Biashara ya Dubai, maarufu kama Dubai Expo 2022. Kuvuma huko kulihanikizwa zaidi na kupaa kimataifa, kutokana na ushiriki wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye siku maalumu ya Tanzania Day.

Miongoni mwa vitu vilivyoifanya kuvuma hadi kileleni mwa dunia ni tangazo la Bendera ya Tanzania na picha ya Rais Samia kurindima kwenye jengo refu zaidi duniani kuliko yote, la Burj Khalifa.

Kwa Watanzania wengi, kwao hii ndiyo mara yao ya kwanza kusikia Tanzania inashiriki kikubwa hivi kwenye maonyesho ya Expo, hivyo kudhani ni mara ya kwanza kwa Tanzania kushiriki maonyesho ya Expo. La hasha! Maonyesho ya Expo yalianzia nchini Japan katika jiji la Osaka na huwa yanafanyika kila baada ya miaka mitano katika nchi iliyoteuliwa.

Tanzania ilianza kushiriki kwa kishindo maonyesho hayo toka mwaka 1970 jijini Osaka yaliyojulikana kwa jina maarufu kama Maonyesho Japan. Tanzania ilishiriki kwa kishindo, na banda la Tanzania likatia fora katika utamaduni. Tulipeleka kundi kubwa la wasanii na bendi za Tanzania, akiwemo Mzee Mayagilo aliyeongoza Bendi ya Polisi. Mzee Morisi Nyunyusa na ngoma zake 10, Mbaraka Mwishehe na Moro Jazz, Mzee Mwinamila na wachezea nyoka, Mbaraka aliporejea akatunga wimbo 'Maonyesho Japan'.

Kwa heshima ya Mbaraka Mwinshehe na Moro Jazz, nikumbushe sehemu ya wimbo huu.

*"Kwanza tunatoa shukurani, kwa serikali yetu ya Tanzania, mutupatia nafasi, ya kwenda Osaka Japan.*

*Kwenye Maonyesho ya ulimwengu, ya mambo ya viwanda na biashara.*

*Mwaka wa 70 banda letu, limesifiwa Japan" x 2*

*Kiitikio*

*" Maonyesho Japan yalifana sana, mataifa yote yalifurahi sana Banda la Tanzania limetia fora, Hoyee"*

*"Maonyesho Japan yalifana sana, Lipembe, Mahoka na ngoma za taifa, Wacheza midimu na wachezea nyoka, Mzee Morisi na ngoma zake 10, Hoyee...*

*Maonyesho Japan yalifana sana, Bwana Mayagilo na Bendi ya Polisi, Wana wa sanaa Juhudi Kuunda Hoye...*

Kwa mantiki hiyo, Dubai 2020, yalikuwa maonyesho ya 13 na hufanyika kila baada ya miaka mitano, hivyo yatakayofuatia yatafanyika mwaka 2025 na yatafanyikia Japan katika jiji la Osaka, yalikoanzia. Kitendo cha Tanzania kushiriki kwa kishindo Dubai Expo 2020, ni uthibitisho kuwa sasa tuna uwezo na tukiamua tunaweza, hivyo sasa maandalizi ya Japan Expo 2025 yaanze mapema.

Jambo la pili, kama Dubai wameweza, sisi Tanzania tukijilinganisha na Dubai, kiukweli kabisa, tunaweza kuomba Tanzania Expo ikafanyika 2030 Dar es Salaam, bahati moja mbaya kwa hizi Expo, hakuna hata moja iliyofanyika nchi yoyote ya Afrika.

Ili Tanzania na Afrika tunufaike na maonyesho makubwa kama haya ya Expo, ni Bara la Afrika kuandaa Expo zetu, hivyo tuendelee kushiriki zingine zote kwa kishindo ili kupata manufaa, wakati tukijipanga kuwa na expo yetu. Hakuna nchi yoyote duniani iliyopata maendeleo ya kweli kwa kuwategemea wafadhili, misaada, mikopo na wawekezaji kutoka nje. Maendeleo ya kweli yataletwa kwa Tanzania kuwajengea uwezo wa ndani watu wake, kutumia rasilimali zetu kama mitaji ili kujiletea maendeleo.

Kuhusu haya mambo ya maonyesho, katika safu hii, nimeishaandika makala tano kuhusu maonyesho. Niliandika kuhusu ushiriki wa TWCC kwenye Maonyesho ya 77, jinsi taasisi ya TradeMark East Africa ambayo ni taasisi ya nje ya Tanzania inavyowasaidia Watanzania kushiriki maonyesho, wakati taasisi za ndani, zikiangalia tu. Kisha nikaandika kuhusu ushiriki wa kusuasua wa wafanyabiashara wa Tanzania kwenye Maonyesho ya Jua Kali yaliyofanyika Mwanza huku nchi jirani zikishiriki kwa kishindo kikubwa kuliko wenyeji Tanzania, na mwisho nikaandika kuhusu Soko huria la Afrika (AfCFTA) kuwa wafanyabiashara wa Tanzania, wasiposaidiwa na serikali, Watanzania tutaishia kuwa watazamaji na masoko ya bidhaa za wenzetu.

Mimi si mchumi wala si mfanyabiashara ila ushiriki mkubwa vile wa Watanzania kwenye maonyesho ya Dubai, umenishangaza. Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye nchi sita na huku tumezungukwa na nchi nane na mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), zenye soko la zaidi ya watu milioni 450.

Kote huku hufanyika maonyesho, sijawahi kusikia Tanzania tukishiriki kwa kishindo hivi. Hizi zote fursa, ambazo Watanzania tukizitumia kikamilifu, zitaleta matokeo chanya kuliko hata Dubai Expo.

Hizo Expo zingine zote 12, si kwamba Tanzania tumekuwa tunashiriki zote ila kwa kupewa kimeza tu na kujibanza kwenye mabanda ya watu. Lakini hii ndio mara ya kwanza kwa Tanzania kushiriki kama nchi kwa kuwa na banda lake na matokeo ndiyo hayo tumeyaona.

Nilishiriki maonyesho ya kimataifa ya utalii yalifanyika New York, Marekani. Kiukweli banda la Tanzania ilikuwa aibu. Sasa mambo yamebadilika. Tuyatumie maonyesho kufanya ujasusi wa kiuchumi badala ya kuendelea kushobokea tu vya wenzetu.

Karibu watoa pongezi wote wanampongeza Rais Samia Suluhu Hassan tu, lakini pongezi zangu zinaanzia kwa Balozi Edwin Rutageruka (Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi), aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE). Huyu ndiye mwasisi wa maonyesho hayo. Pongezi pia ziende kwa Wizara na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) waliopokea wazo na Rais ambaye alipotia tu mkono wake, ushiriki wetu ukawa kama umetiwa hamira, ukaumuka.

Kwa vile kuna maonyesho mengi na kupitia Dubai Expo Tanzania tumeonyesha tunaweza, natoa wito kwa Mama, TANTRADE na Wizara ya Viwanda, tushiriki maonyesho mengine yote kwa nguvu ile ile kama tuliyoonyesha Dubai.

**Mungu Ibariki Tanzania,**
**Kazi Iendelee.**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Chonde chonde wanyama kuchukua nafasi zetu!



Na Joseph Kulangwa

**Hivi itakuwaje mathalan siku moja unaamka unakuta kundi la simba na tembo nje likitaka uondoke uliachie nyumba yako na mali zako ili liishi hapo nawe utokomee porini na kuanza kuwindwa?**

KUNA miaka fulani nyuma huko, nilipata kuandika mahali jinsi dunia itakavyobadilika na binadamu kubadilishana makazi na wanyama, sikueleweka kwani wengine walidhani nimegeuka zombi na wengine taahira.

Nilisema wakati huo kwa mwangwi wa kutabiri kwamba hawa wanyama tunaowafukuzia kila siku za sikukuu eti kusindikiza sherehe zetu kwa kuwageuza visusio, wanatuangalia tu kuwa iko siku tutabadilishana majukumu.

Wakati mwingine huwa nawashukuru Wamasai wa Ngorongoro kuwa pengine walinielewa, walipoamua kuishi na wanyama wafugwao na wanyama pori kishikaji kabisa, tena bila kudhuriana.

Wakafika mbali zaidi, wakaona ni vyema kukutanisha ng'ombe, mbuzi na kondoo na pundamilia na swala, wakala majani pamoja bila kugombana. Nikaamini kwamba hawa walielewa kuwa iko siku uliyemtendea mabaya, atakuja kukurudi tu.

Hivyo basi, siku zitakapofika za wanyama kuchoka kuishi maporini huku binadamu tukiishi mijini tukijisikia tukienda porini kuwaua kwa jina la kuwinda na wale wa nyumbani tukiwachinja kwa kisingizio cha sikukuu, watafanya mapinduzi.

Hivi itakuwaje mathalan siku moja unaamka unakuta kundi la simba na tembo nje likitaka uondoke uliachie nyumba yako na mali zako ili liishi hapo nawe utokomee porini na kuanza kuwindwa?

Itakuwaje wakitokea miongoni mwa hao wanyama wakakuhurumia na kukutaka ubaki lakini uwe mfugo wao, ili siku za Krismasi, Iddi na Pasaka wakuchinje washerehekee Maulid na kuzaliwa kwa Kristo wao?

Nimekuwa nikijiuliza haya na kukosa majibu na mwishowe kuacha tu na kukubali dunia iendelee kuzunguka bila kusimama, ili siku ya siku ifike, nishuhudie mapinduzi hayo ya kukata na shoka. Mnyama mjini, binadamu porini!

Ingawa nitakuwa mmoja wa waathirika, naamini nitakuwa nimeshajiandaa kisaikolojia baada ya maono haya yanayozidi kutokea duniani, hususan Tanzania ambako sasa mauaji ni kama sehemu ya maisha, lakini pia Ukraine ambako Putin kaamua kuwa na kichwa cha puto na kuua wenzake.

Hebu tazama kila kona ya nchi yetu hii yenye utulivu na amani, watu wanaua, wanauana, wanauawa na wanajinyonga! Ukiwasikiliza makamanda wetu wa Polisi katika mikoa yanakotokea haya, unaambiwa ama ni wivu, ni ushirikina, ni ukata ni msongo wa mawazo!

Porini waliko wanyama, hawauani uani hivi ila kwa ekolojia, wanyama hawajinyongi, wanyama hawajiui. Hatujapata kusikia hata fisi ambaye ni mkorofi kwamba kakutwa amening'inia kwenye mti kwa kamba ya gamba la mti.

Siku zote tunasema wanyama hawana akili na hata wakati mwingine tukitukana wanetu kuwa huna akili kama ng'ombe, angalia fisi huyu na matusi ya kila aina, mbwa sijui nini! Lakini kwa hili la kuuana bila sababu au kwa kuamini ujinga wa mapenzi na kurogana, wanyama hawana.

Nani sasa mwenye akili hapo, mnyama au binadamu? Eti mtu ana kifafa chake huko, mara anamvamia baba yake na kumkatakata mapanga eti ndiye kamroga! Inashangaza kwa kweli.

Dume linatoka zake huko limekandikwa maneno kichwani na kuamini, linafika nyumbani linachukua panga na 'kumghecha' mkewe mpaka kumuua, kisa eti limeambiwa 'anatembea' na wanaume wengine!

Kwa tabia na akili kama hizi, hivi kwa nini tusibadilishane makazi na wanyama nasi tukafakamie majani huko porini, badala ya kuishi kwenye nyumba za kifahari, lakini tusitumie hata huo ubongo kidogo tuliowekewa kwenye mafuvu na Mungu, kwa mambo chanya?

Angalia binadamu tunachukiana na kutungiana uongo hata kufikia kubambikiana kesi mahakamani, zisizo na miguu wala kichwa, polisi nao tunakutana barabarani huko tukipishana lugha tu, tunabambikiwa kesi za bangi na mauaji!

Mnyama hana hizo, ataua ili apate riziki, hata siku moja hataua eti kwa kumwona mwenziwe kanenepa, la hasha! Atapambana apate nyama, apate majani kwani ndivyo alivyoumbiwa na Muumba wake ili kujipatia riziki.

Hakika tusipobadilika, tujiandae nafasi zetu kuchukuliwa na wanyama, ili nasi tufike wakati tubweke kama mbwa na kunguruma kama simba porini kutokana na dhambi tunazojichumia wenyewe. Kumbukeni Mungu hana upendeleo, sote tu viumbe wake na Dunia yote ni yake, hivyo kila kiumbe kina haki ya kuishi kokote.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Bonde la Maji Kati mfano mzuri kuigwa utunzaji yanzo vya maji



Na Thobias Mwanakatwe

NI Februari 28, 2022 saa 3:00 asubuhi naianza safari kutoka Karatu mjini kwenda Kata ya Mang'ola wilayani Karatu mkoani Arusha kwa ajili ya kuhudhuria uzinduzi wa mradi wa uhifadhi na utunzaji chanzo cha maji cha chemchem za Qang'dend na mito ya Baray na Mang'ola.

Katika uzinduzi huo ambao mgeni rasmi ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, baada ya kufika katika kijiji cha Qang'dend, nawaona viongozi wa Bonde la Maji Kati, wizara, serikali ya mkoa wa Arusha, wilaya ya Karatu, tarafa, kata na wananchi kwa ujumla kila mmoja akiwajibika kwa ajili ya maandalizi ya shughuli hiyo.

Kama ilivyo kawaida, anapokuja kiongozi mkubwa wa kitaifa kwa shughuli yoyote ile, viongozi wa chini kila mmoja anakuwa na kawasiwasi kwamba sijui atasema nini. Wengine wanafika mbali kwa kuwaza kuwa huenda atamtumbua mtu.

Wasiwasi huo ni wa kawaida lakini naweza kusema siku ya uzinduzi wa mradi huo, hata kama kulikuwa na kapresha fulani, haikuwa kubwa kwa sababu shughuli nzuri ilikuwa imefanywa katika utekelezaji wa mradi huo.

Nadiriki kusema fedha zimetumika vizuri kutokana na usimamizi mzuri wa viongozi na Bodi ya Bonde la Maji Kati chini ya Danford Samson ambaye siku ya tukio, nyota ilimuwakia na kupandishwa cheo kuwa Ofisa wa Maji Bonde la Kati. Kabla ya hapo, alikuwa akikaimu nafasi hiyo.

Waziri Aweso aliamua kumpandisha cheo kwa sababu katika kipindi ambacho amekuwa akikaimu, amefanya kazi nzuri na ya kizalendo katika usimamiaji wa miradi.

Sote ni mashahidi. Katika baadhi ya maeneo kumekuwa na tatizo la viongozi kwenye usimamizi miradi ambayo serikali inatoa mamilioni ya fedha kama si mabilioni. Hii inatokana na tamaa na kukosa uzalendo ndiyo maana baadhi ya viongozi wanaingia kwenye ufujaji fedha, hivyo kuwafanya viongozi wa kitaifa kuchukua uamuzi mgumu dhidi yao.

Viongozi na bodi ya Bonde la Maji Kati, hakika wametoa somo kwa watendaji wengine ndani ya serikali. Siku ya uzinduzi huo, Mkurugenzi wa Raslimali za Maji, Dk. George Lugomela, alimweleza Waziri wa Maji kuwa Bodi ya Maji Bonde la Kati katika mradi huo imeokoa Sh. milioni 422 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa uhifadhi na utunzaji chanzo cha maji cha chemchem za Qang'dend na mito ya Mang'ola na Baray.

Hatua ya Bonde la Maji Kati kuokoa kiasi hicho cha fedha, imenipa msukumo wa kusema viongozi wa bonde hili ni wazalendo wa kweli kutokana na usimamizi mzuri wa fedha. Hapa ndipo nadiriki kusema mabonde mengine yaige mfano huo kwani fedha zinazotumika kujenga miradi ni jasho la Watanzania, hivyo inapotokea mtu mmoja anazifuja, anakuwa amewakwaza wananchi wengi.

Ni imani kwamba Samson kwa uaminifu aliouonyesha na hatimaye kuthibitishwa na kupewa nafasi hiyo, atalifikisha mbali bonde hilo kimaendeleo na si tu katika usimamizi wa miradi bali pia utunzaji wa vyanzo vya maji.

Nakumbuka Dk. Lugomela alisema hapa nchini kuna vyanzo vya maji 1,867 ambavyo vinatoa huduma lakini viko katika hatari ya kuharibiwa. Akaenda mbali zaidi kwa kusema vyanzo vya maji ambavyo vimewekewa mipaka ni 180, vilivyotangazwa katika gazeti la serikali na kupata GN ni 18 na vyanzo 45 viko kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali vikisubiri kutangazwa.

Kubwa zaidi, Waziri Aweso alisema asilimia kubwa ya viongozi na hata wananchi wanajua umuhimu wa kujengewa mradi tu lakini wanasahau suala la kulinda na kutunza vyanzo vya maji.

Alisema haiwezekani shughuli za binadamu zinafanyika katika vyanzo vya maji na hatuwezi kuona uchimbaji madini unafanyika katika vyanzo vya maji na mtu wa bonde yupo tu ofisini amekaa hawezi kuona badala ya kushirikisha jamii na viongozi wa eneo husika.

Aweso aliweka bayana kwamba haipendezi wala haifurahishi kuangalia katika luninga (TV) mwananchi ameshalima mazao yake kwenye chanzo cha maji halafu ofisa wa bonde anakwenda na panga kuyakata kwa sababu wakati mwananchi analima huyo ofisa alikuwa wapi.

Waziri alisema miaka ya nyuma maeneo mengi yalikuwa na chemchem za maji lakini leo hazipo, zimekauka kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira unaofanywa na baadhi ya wananchi kwa kulima katika vyanzo vya maji na kuendesha shughuli za ufugaji.

Matamko haya ya viongozi wa kitaifa yenye msisitizo mkubwa, yanatukumbusha sote kuhakikisha tunalinda vyanzo vya maji kwa kukemea kwa nguvu zote wanaojaribu kufanya uharibifu wa vyanzo hivyo.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@ yahoo.com au simu: 0747-364444**

## DARASA LA NDOA

# JE, FEDHA NI BARAKA AU LAANA KATIKA FAMILIA? -2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala hii, ilielezwa kuwa fedha ni njema na mtu kuwa nayo si uovu wala dhambi lakini nafasi unayoipa katika maisha yako ndiyo itakayoamua kama ni baraka au laana.

Ni dhahiri kwamba fedha ni baraka ikitafutwa kwa halali na kutumika vizuri, kwani inaweza kuwa nyenzo ya kuleta maendeleo pale itakapotumika vizuri kwa mambo yenye manufaa. Hata hivyo, fedha ina uwezo wa kuleta maumivu na kugeuka kuwa shina la ubaya isipotumika vizuri.

Ziko baadhi ya ndoa zilizoimarika baada ya kupata fedha na wanandoa kufurahia mafanikio yatokanayo na fedha zilizopatikana. Lakini zipo ndoa zilizoharibika mara baada ya fedha kuingia. Baadhi ya wanandoa hawafurahii maisha ya ndoa pamoja na kwamba wanazo fedha. Fedha imegeuka kuwa kama kirusi kinachoharibu ndoa na uhusiano wa wanandoa.

Sehemu hii ya pili na ya mwisho inaweka bayana nini kifanyike ili fedha iwe baraka na kuleta ustawi katika ndoa na familia. Kwa mantiki hiyo, mambo yafuatayo, yanapaswa kuzingatiwa ili iwe Baraka;-

**MIPANGO NA NIDHAMU YA FEDHA**

Mafanikio ya kiuchumi ya mtu yeyote yanahitaji mipango na nidhamu katika fedha. Watu wengi hushindwa kufikia malengo na kufurahia maisha kwa sababu ya kukosa mipango na nidhamu ya fedha. Mpango wowote huanzia kwenye kipato kidogo, si lazima kuwa na kipato kikubwa.

Tabia nzuri ya kujenga na kuiendeleza tangu mwanzo wa ndoa ni ile ya kujipangia bajeti ya familia. Hii husaidia kuelewa ni fedha kiasi gani zinapatikana na kupanga jinsi gani zitatumika. Katika kufanya hivyo, ni kanuni kuwa matumizi ya fedha yasizidi kipato.

Wanandoa wanapaswa waishi kulingana na kipato chao na uwezo wao. Wajilinde dhidi ya mashinikizo na tamaa ambavyo huweza kusababisha waishi maisha yasiyo yao. Moja ya mambo yanayochangia uwapo wa amani na mafanikio katika ndoa ni kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha.

**KUWAFUNDISHA WATOTO**

Watoto wasipewe fedha nyingi za kutumia shuleni kila siku. Ni muhimu watoto wafundishwe kuwa si wakati wote wanaweza kupata wanachotaka. Kadri wanavyokua, waelekezwe kuwa na nidhamu ya fedha na shukrani kwa Mungu.

Ikumbukwe kuwa, wale tunaowaona kuwa ni watoto leo, siku zijazo watakuwa ni watu wazima wanaopaswa kujitegemea katika maisha. Maisha wanayoishi leo ni taswira ya maisha yao ya hapo baadaye. Kila mzazi atavuna alichopanda na kuwekeza kwa mtoto wake.

**USIRI KUHUSU VIPATO**

Kumekuwa na tabia ya usiri mkubwa miongoni mwa wanandoa juu ya vipato vyao. Wanandoa wengi hawashirikishani kuhusu vipato vyao hatua ambayo imesababisha uwazi na ukweli katika mambo ya fedha kumekosekana katika maisha ya wanandoa wengi ama kwa kukusudia au kukosa ufahamu. Hali hii imekuwa ikichangia uwapo wa migogoro katika ndoa nyingi, hasa pale mke au mume anapogundua kuwa alifichwa kuhusu jambo fulani.

Hali hii inapojitokeza, huondoa tumaini (trust); hudumaza pendo la ndoa na mapenzi; hupoteza hisia chanya, mvuto na kuondoa uhai wa ndoa. Mahali pengine, usiri juu ya vipato umeleta mahangaiko na maumivu makubwa hasa pale mmoja wa wanandoa anapofariki dunia.

Kwa kuzingatia maana halisi ya ndoa na misingi yake, wanandoa wanapaswa kushirikishana na kuelewana juu ya vipato vyao ili kuepuka matatizo yasiyo ya lazima. Ni muhimu wanandoa watengeneze mazingira ya uwazi na ukweli juu ya fedha na mali zao. Wafikirie athari zinazoweza kutokea kutokana na maamuzi ya kuwa wasiri kwa waongo miongoni mwao.

**KUISHI KWA UMOJA**

Kuishi kwa umoja na mshikamano ni moja ya misingi ya ndoa bora. Hata hivyo, wako wanandoa wanaofanya vitu au mambo yao pasipo umoja wala mshikamano. Mfano, imetokea mahali pengine kwamba, mke au mume anaweza kununua kiwanja, kununua gari, kujenga au kununua nyumba, kukopa fedha benki, kusaidia ndugu kifedha au kuanzisha mradi fulani bila mwenzi wake kujua.

Inapogundulika, hali hii husababisha masononeko na mgogoro mkubwa. Yafaa mume na mke waishi kwa umoja na mshikamano kwani hii huleta maana halisi ya wao kuwa wanandoa.

**KUPENDA MAZUNGUMZO**

Wanandoa wazungumze kuhusu tofauti zao na kushirikishana hisia walizonazo kwa lengo la kusaidiana na kurekebisha hali iliyopo. Kuishi na machungu moyoni huathiri afya ya akili, mwili hata kusababisha kifo. Kuweka vinyongo moyoni hushawishi visasi. Siku zote vinyongo na roho ya visasi si njia nzuri ya kutatua tatizo.

Hali hii huwa haileti suluhu, bali huongeza maumivu, huondoa utu na uwepo wa Mungu katika maisha ya mtu. Moja ya mambo yanayochangia watu kuumizana na mauaji ya kikatili katika familia na jamii yetu ni uwapo wa watu wenye vinyongo ambao hukusudia kulipiza kisasi kwa wenzao.

Ili kuepukana na matatizo kama haya ni muhimu wanandoa wadhamirie kujenga tabia ya kupenda kujadiliana kwa upendo na upole na kushauriana kwani mazungumzo hujenga uhusiano na familia bora. Pale wanandoa wanaposhindwa kushughulikia tofauti zao, ni busara kuomba msaada wa viongozi wa dini au washauri wengine wenye weledi ili kutunza ustawi wa ndoa, familia, afya njema ya akili, mwili na roho.

**■ Mch.Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

MACHI 6, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

## Samaki wa kupaka mlo tosha




## MITINDO

Kapelo zinavyopagawisha vijana




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# NYUSI ZINAZOITA

# Mwanamke anang'arishwa na wanja

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | S | H | A | K | A |
| ■ | H | ■ | ■ | O | ■ |
| L | I | A | ■ | K | ■ |
| ■ | N | ■ | T | O | A |
| ■ | D | ■ | ■ | T | ■ |
| T | A | M | B | O | ■ |


## AMSHA AKILI



## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
INA, UNA, PANDE, ZIBIA, IKINGE, ZENGEA

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

MTOTO John, alichukua redio kwao na kuamua kuipeleka kwa fundi kutokana na kutaka kuwajua watangazaji wanaosikika.

Alipofika kwa fundi John alimkabidhi na haya yalikuwa mazungumzo yao.

John: Fundi nimeleta redio ya baba ili uitengeneze

Fundi: Ina matatizo gani?

John: Watangazaji wanasikika sauti zao lakini hawaonekani

Fundi: Redio ni nzima na watangazaji hawakai ndani ila humu kuna vyombo vinanasa mawimbi ya sauti tu.

John: Kumbe hivyo! Mi nilijua wamo ndani

**SWALI**

Zao la mpunga linalimwa mkoa gani kwa wingi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Marafiki unaopaswa kuwa nao ili ufanikiwe

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vyetu vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo nijadili kuhusu aina za watu au marafiki unaopaswa kuwa nao ili ufanikiwe.

Katika maisha tunayoishi, si kila mtu unapaswa kuwa naye. Si kila mtu aliyeko duniani ni rafiki yako. Kuna aina za watu unapaswa kuwa nao ili ubarikiwe na kufanikiwa.

Pia si kila baba ni baba yako, wala si kila mama ni mama yako. Au naweza kusema si kila sketi ni mke wako na wala si kila suruali ni mume wako.

Vile vile si kila madhabahu ni madhabahu yako. Si kila mahali pamebeba baraka zako. Mungu anakuweka eneo fulani kwa sababu ndipo zilipo baraka zako, pana utukufu wako na heshima yako.

Kumbuka, Mungu ndiye anayetupatia marafiki au watu wa kuwa nao kwa kuwa yeye ndiye anayewajua. Kuna watu unapaswa pia kuachana nao ili ufanikiwe. Wako watu hupaswi kuwa nao karibu kwa hali yoyote ile ili uwe salama.

Ni kweli aweza kuwa mwenzako na unampenda, si umchukie lakini pia si lazima awe rafiki yako. Mungu anasema hivi katika moja ya maandiko yake: "Kwa kuwa ulikuwa wa thamani machoni pangu na mwenye kuheshimiwa, nami nimekupenda; kwa sababu hiyo, nitatoa watu kwa ajili yako; na kabila za watu kwa ajili ya maisha yako."

Mungu ndiye anayetupatia watu wa kuwa nao. Wengi tunapata hasara kwa sababu tunawachukua watu sisi wenyewe. Utasema huyu anacheka cheka sana, basi ndiye mtu wangu. Lakini Mungu anasema ukimpenda, atatoa watu kwa ajili yako!

Ni kweli binti anataka kuolewa, lakini je, huyo mume Mungu ndiye aliyekupa? Na huyo mke una hakika Mungu ndiye kakupatia? Jiulize, hautaishia njiani na kufeli. Huyo rafiki una hakika ni Mungu kamleta kwako?

Si kila anayekusogelea anapaswa kuwa rafiki yako, hapana! Rafiki anapaswa aletwe na Mungu na hakika, hatakuacha njiani wala kukuumiza, wala kukung'ata. Wengi wamepata hasara kwa sababu wameamini watu feki. Shetani anaweza kukuletea mtu feki akaja karibu yako, akatwaa talanta yako akaondoka nawe ukabaki unalia.

Wako watu wengi sana walimwamini rafiki, halafu huyo rafiki akampindua na kumchukulia mume wake! Utasikia mtu anasema; 'Rafiki yangu, shoga yangu mzuri, twende kwangu mimi nimechumbiwa, mchumba wangu mzuri yupo, twende ukamuone'.

Alipokwenda kumuona anasema, aisee, huyu lazima nimpate. Anamzunguka baadaye anambeba anakuwa naye. Mwenye mchumba anapogundua hila ya rafiki yake anaishia kulia, kumbe alikuwa ni rafiki feki.

Msomaji wangu, Mungu ndiye anapaswa akuletee rafiki au mtu wa kuambatana naye. Na anapokuja ni lazima ujiridhishe kwamba, je, huyu ameletwa na Mungu? Yule aliyeletwa na Mungu atakusaidia, atakutia moyo, hatakuaibisha wala kukutoa machozi ya huzuni!

Wako watu walikuwa na tabia nzuri wakaharibiwa na marafiki. Ulikuwa mtii, mnyenyekevu unayempenda Mungu sana, lakini ukakutana na marafiki wenye tabia mbaya na vyote hivyo vizuri vikatoweka ndani yako.

Kuna rafiki unaweza kuwa naye ukashangaa unashindwa kufanya mambo fulani ya kimaendeleo. Mwingine anakukatisha tamaa unapomshirikisha jambo fulani la kubadilisha uchumi wako.

Rafiki mwema atakuongoza pema, rafiki mzuri atakusaidia ufike mbinguni. Na rafiki mzuri ni yule atakayekusaidia ujisahihishe, atakupenda. Jiulize, unahakika na rafiki yako?

Kuna watu wataonekana kwa nje wamevaa ngozi ya kondoo, lakini ndani ni mbwa-mwitu wakali. Kuna watu ukiwaangalia mdomoni ni malaika lakini mioyoni mwao ni mashetani.

Unaweza kuwa na rafiki lakini vile unavyoongea ukiwa naye, sivyo anavyokuongelea unapokuwa haupo naye. Huyu usipokuwa naye, akikuta unasemwa, yeye anaongezea.

Utasikia mtu anajihami kwa kusema; eti walipokuwa wanaongea, mimi nilinyamaza kimya. Kuna watu wanaweza kuletwa na mashetani wakajipenyeza wakaingia au wakaharibu maisha yako pasipo wewe kujua.

Msomaji wangu, bila shaka umejifunza kitu kwa elimu niliyotoa hapo juu kuhusu marafiki. Ni vema kumuomba Mungu akuletee watu wazuri. Wale ambao hawatasema uongo watakuambia ukweli.

***Tutaendelea wiki ijayo na mada hii ya marafiki. Je, una maoni au kisa? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581 .***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Tumepiga hatua maendeleo ya mwanamke, tusonge mbele zaidi

"HAKI sawa kwa maendeleo endelevu" ndiyo kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yatakayofanyika Machi 8, mwaka huu, ikiwa na msisitizo kuwa kila mwanamke ana haki ya usawa kwenye nyanja mbalimbali na maendeleo endelevu.

Kwa mujibu wa kamusi, haki ni jambo ambalo mtu anastahili au anachostahili kuwa nacho. Inapoondolewa ndiyo kunyang'anya au kupora haki ya mwingine.

Tangu enzi na enzi, mwanamke ameachwa nyuma kutokana na mfumo dume uliomkuza ambao ulijitengenezea mazingira ya kutawala na kumiliki, huku hata kile kilichozalishwa na mwanamke kiliendelea kuwa mali ya jinsia nyingine bila kujali umri.

Mila, utamaduni na desturi za kila jamii zilitumia kila nafasi kuweka utaratibu ambao ukiufuatilia kwa kina ulilenga kuumiza jinsia moja na kutoa upendeleo kwa nyingine hata kwa mambo ya haki ambayo ni stahili au anachostahili mtu.

Mathalani, baadhi ya makabila mwanaume huoa wanawake wengi kwa lengo la kupata nguvu kazi ya watoto ambao hushirikiana kuzalisha kwenye kilimo na mifugo lakini mwenye uamuzi wa kilichozalishwa ni mwanamume ambaye anaweza kuamua kuongeza mke mwingine au kutumia kwa starehe na familia haitakuwa na nguvu ya kuhoji lolote.

Wengine wanapojaliwa watoto wa kike huamini mali imeongezeka kwenye familia, baada ya kuwakeketa, huwaozesha kwa nguvu ili kupata mifugo kuongeza mali maana yake hawana haki ya kuendelea na masomo.

Kama mama yake hakusoma maana yake hata mtoto hasomi,inakuwa ni mwendelezo wa wanawake wa baadaye ambao hawakupata fursa ya elimu ambayo ni haki kwa mujibu wa sheria.

Kutokana na hali hiyo, katika mnyororo wa maendeleo huwakuti wanawake kwenye nafasi za juu za uongozi na uamuzi kwa kuwa hawakupata nafasi ya kujiendeleza. Matokeo yake wanaendelea kutawaliwa na kutokuwa na nguvu kiuchumi.

Licha ya changamoto nyingi, jitihada zimefanywa na asasi zisizo za kiserikali na serikali kuelimisha jamii kuachana na mfumo dume,kuwa na sera na sheria zinazowalinda wanawake na mtoto wa kike hasa katika elimu.

Wako ambao wamepambana wenyewe kwa jasho na damu kufikia maendeleo au nafasi fulani kwenye taasisi, mashirika na serikalini, baada ya kuwapo wamesaidia kuinua wanawake wengine,kupaza sauti na kupigania haki za wanawake na watoto.

Tunapozungumzia maendeleo endelevu tunahusisha na malengo 17 ya maendeleo ya milenia ambayo kila moja limeweka malengo mahususi ya kufikiwa, huku kila nchi, Tanzania ikiwamo, imeridhia kutekeleza kwa vitendo.

Kwa sasa, Tanzania tunajivunia kwamba kwa miaka 60 ya Uhuru sasa tuna Rais mwanamke ambaye anaongoza kwa mfano na sasa mtazamo hasi dhidi ya wanawake unaendelea kupungua na itafika wakati utatoweka kabisa.

Kwa sasa si jambo la ajabu kukuta mwanamke ni mwenyekiti wa bodi, waziri, mkurugenzi wa taasisi fulani au nafasi kubwa ya uamuzi. Wengi wanafanya vizuri na kutuma ujumbe kuwa mwanamke ukimwamini na kumpa nafasi anasimama vizuri kwenye majukumu yake.

Wako waliokuwa na wasiwasi kuwa sasa itakuwaje nchi inaongozwa na Rais mwanamke, kadiri siku zinavyokwenda wasiwasi wao unaendelea kufifia, mambo mengi ya maendeleo na umoja wa nchi yanaendelea na sasa kuna mtu wa mfano ambaye anasaidia watoto wa kike kujiamini kuwa inawezekana.

Katika kusherehekea siku hii ni muhimu sana kuhakikisha jinsia zote zinashiriki mchakato wa maendeleo pasipo kuacha yeyote nyuma, kwa kuwa maendeleo yanategemea wote na haki au usawa unaopiganiwa ni kwa ajili ya wote pasipo kuumiza yoyote.

Lazima tujenge jamii ambayo kila mmoja atafurahia kuishi humo na kufanya maendeleo pasipo kikwazo kutokana na jinsia yake aliyopewa na Mungu. Wote tumeumbwa kwa mfano wa Mungu maana yake sote tunaweza kutoa mchango kwa nchi yetu kwa maendeleo endelevu.

Baadhi ya mila na tamaduni zililenga kudumaza jinsia moja na kuipa nguvu nyingine kwa malengo mahususi, ilisahaulika kuwa maendeleo yoyote yanategemea jinsia zote.









Ndafu ni chakula muhimu katika harusi za baadhi ya makabila, lakini utamaduni huu unapotea kwa kasi na badala yake wengi wanapenda kutumia keki. Pichani ni baadhi ya harusi zilizopambwa na matumizi ya ndafu na kupendeza zaidi.

# MITINDO

a Mwakangale




# Kapelo zinavyopagawisha vijana

KWA wanaume wanaojali na kuthamini mavazi wanafurahia pale wanapokuwa tofauti kila wakati.

Sanaa ya mitindo ya mavazi inapendeza zaidi kama mtu husika atajua nini anataka na kwa wakati gani katika kupangilia nguo na vitu vingine.

Baadhi ya wanaume wanafanya chaguo zuri pale wanapovaa kofia na mara nyingi utakuta wakibadilisha aina mbalimbali za kofia zikiwa na mitindo tofauti.

Wataalamu wa masuala ya mitindo wanasema uvaaji wa kofia pamoja ni moja ya njia ya kupendezesha sura. Pia husaidia kulinda nywele kuathirika na miale ya jua.

Je kofia gani zinazopendekezwa kuvaliwa na wanaume kwa ajili ya kumfanya awe na muonekano wa kipekee?.

**KAPELO**

Kofia aina ya kapelo ina mwonekano mzuri na huwafanya vijana wengi kupenda kuvaa katika shughuli zao za kila siku.

Kwa kawaida kofia ya kapelo haichagui aina ya nguo, lakini ni vizuri ikatumika na nguo zinazoendana nazo pamoja na zile zinazokwenda na wakati.

Kofia ya aina hii hairuhusiwi kuvaa sehemu za kazi au ofisi za kiserikali na kama zikitumika inakuwa katika shughuli maalum za kitaifa, kisiasa, kitamaduni na kijamii.

Hata hivyo kundi la vijana hasa wasanii wamekuwa wakivaa na kuzidisha mvuto wa vazi hilo kwa watu wengine.

**UNAPONUNUA**

Wakati unapofikiria kununua kofia ya Kapelo, hakikisha unakuwa makini kwa kuangalia ubora wake na rangi unayopenda.

Hakikisha ukubwa wa kofia unalingana na kichwa chako, usinunue kubwa kwani haitakuletea matokeo mazuri. Pia kofia isikubane sana na kukuletea usmbufu pale unapovaa.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# NYUSI ZINAZOITA
## Mwanamke anang'arishwa na wanja



JAMBO muhimu katika kujiremba sura ni kupaka nyusi wanja mweusi.

Wanja mweusi ni pambo kuu katika kuujenga uso katika mwonekano wa kuvutia na wenye bashasha kwa mwanamke.

Wataalam wa urembo wanasema wanja unabeba asilimia zaidi ya 50 katika kuupendezesha uso.

Endapo ukikosea kupaka wanja, basi jua mapambo yako ikiwamo 'makeup' utaonekana mbaya.

Unaweza kupaka wanja kwenye nyusi kwa kutumia vifaa maalumu vya kupakia ambavyo vimekatwa ukubwa wa nyuzi ili kurahisisha kazi.

Pia unaweza kupaka wanja kwa kufuata muundo wa nyusi zako asilia na kisha kusawazisha kwa kutumia 'concealer' ili uweze kupata wanja ulionyooka na unaopendeza

Kumbuka kuchana nyusi zako baada ya kupaka, lakini tambua nyusi ni kama pacha ni muhimu kuhakikisha unalingana kwenye nyusi zote mbili.

Hakikisha usinyoe nyusi zako zote bali zipunguze tu kidogo ili kuzitengeneza ziwe na muonekano mzuri, hii itasaidia kufanya wanja wako uonekane asilia zaidi.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Samaki wa kupaka mlo tosha

WAKATI mwingine mtu unakuwa umechoka na usingependa kupoteza muda jikoni, kwa mlo wa haraka inakuwa ni wazo zuri.

Mlo huu ni rahisi kuuandaa na hata haikuchukui zaidi ya dakika 20 chakula kinakuwa tayari mezani.

**Mahitaji**

Samaki, viazi mbatata kiasi, Lettice kiasi, nyanya za maji, limao moja, kitunguu swaumu, chumvi na mafuta ya mzaituni.

Matayarisho

Mchanganye samaki na chumvi, swaumu na nusu ya limao kisha muweke pembeni.

Baada ya hapo washa oven kisha tia viazi mbatata zilizokatwa vipande mduara zikisha karibia kuiva anza kumpika samaki.


Tia mafuta kidogo sana kama kijiko kimoja cha chai hivi ikisha pata moto kiasi muweke samaki wako (upande wenye ngozi chini kwanza).

Mpike mpaka uone rangi ya kahawia kwa chini kisha mgeuze upande wa pili, huku samaki wako akiwa anaendelea kuiva, tayarisha salad. Chakula chako kitakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Usikurupuke kuuza nyumba

BIASHARA ya nyumba na uwekezaji wa majengo ya kisasa inaendelea kushika kasi kila siku, si Tanzania tu bali duniani kote.

Lengo kuu la makala hii ni kupeana maarifa kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kuuza nyumba kwa kujitathmini na kufanya uamuzi sahihi.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Christian Kamase, anasema miongoni mwa mambo ya kuzingatia kabla ya kufikia uamuzi wa kuuza nyumba, ni lazima utathmini lengo au sababu kuu ya kufanya hivyo na siyo kukurupuka.

Anasema wakati tulio nao, biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo vinafanyika kwa mbinu za kisasa ambazo ni matokeo chanya ya ukuaji wa sekta hiyo ya ujenzi inayotokana na mapinduzi ya teknolojia mbalimbali duniani kote.

"Watu binafsi, kampuni na taasisi nyingi zimejitokeza kwa wingi kuzitumia fursa zinazoendelea kujitokeza kila siku kwenye biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo hususani kwa kuiendesha kisasa zaidi kwa kutoa huduma za makazi na biashara kwa wadau mbalimbali," anasema Kamase.

"Lakini kuna baadhi ya watu wamejikuta wakiingia kwenye uuzaji wa majengo au nyumba kutokana na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo kwenye maisha, ndiyo maana ninashauri kwamba ni muhimu sana ukajitathmini kabla ya kuuza nyumba yako," anasisitiza.

Moja ya mambo ya kujiuliza, kwa mujibu wa Kamase, ni je, ni kwa lengo la kibiashara au kutokana na kushindwa kukabiliana na msukosuko wa changamoto za maisha zinazokukabili?

"Kwa mfano Januari ambayo inajulikana kwa misukosuko ya kifedha, kwa hiyo mtu bila kutulia na kujitathmini, unaweza kujikuta unafanya uamuzi wa majuto baadaye," anasema.

Jambo lingine anasema endapo kuna ulazima wa kuuza, ni vyema kabla ya kufanya uamuzi huo, kutathmini bei na gharama ya mauzo ambayo unapeleka sokoni ili kukusaidia kufahamu kiwango halisi na faida au mapato utakayopata kwa kutimiza malengo unayokusudia.

Mtaalamu huyo anashauri kwamba ni muhimu kuzingatia kwa kuhakikisha nyumba yako inakuwa na muonekano mzuri wa kushawishi wanunuzi na kwamba kama rangi yake ilikuwa imechakaa, ni vyema kuipaka upya pamoja na kuzingatia kuwa inakuwa safi wakati wote.

Anasema mvuto wa nyumba nao utakusaidia kukuongoza pia katika namna ya kufanya tathmini ya bei na itasaidia inunuliwe kwa muda mfupi.

Pia anashauri kwamba kabla ya kufanya uamuzi wa kuuza, ni vyema kutathmini hali ya soko la nyumba badala ya kukurupuka.



## Namna ya kuchagua jiko la gesi



IDADI kubwa ya watu wanapenda maisha ya kisasa, na moja ya vitu vinavyolingana na maisha hayo ni uwepo wa jiko la gesi ndani ya nyumba.

Jiko la gesi linaharakisha upikaji wa chakula na kuepukana na uharibifu wa nyumba kutokana na moshi.


Lakini unapotaka kumiliki jiko hilo lazima uzingatie mambo mbalimbali muhimu na baadhi ni haya yafuatayo.

1: Hakikisha unaamua kiwango cha bei ambacho unaweza kununua kulingana na ubora na kampuni iliyotengeneza.

2: Amua juu ya mtindo wa jiko, kulingana na muundo na vifaa vya ndani vya jiko ambalo umelichagua.

3: Angalia aina ya jiko unalotaka kama vile jiko moja, mawili hadi manne. Uchaguzi hutegemea kiwango cha chakula kitakachopikwa. Unapaswa pia kuzingatia utendaji mzuri wa tanuri la kupikia. Hakikisha ubora wa njia za kupikia, idadi ya sinia, na uwepo wa trei kwenye jiko.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
'UGHAIBUNI WAACHE WAZICHAPE WAKICHOKA TUNAINGIA MAJESHI YA AKIBA KUFUNGA KAZI
CHIM-PUMU
TANDALE KWA MFUGA MBWA
SI UMESEMA MWENYEWE HUNIPENDI...
NITAJIE KWANZA 'PASIWEDI' ZA KADI ZAKO ZA BENKI ALAFU RUKSA KAJIUE
TUSIBISHANE BHANA! JANA HAMJAFANYA DORIA NISINGEPIGWA VILE NA MKE WANGU USIKU KUCHA BILA KUOKOLEWA...HAPA NILIPO MASIKIO YAMEZIBA "NIMEBURUZWA HASWA!"
BADALA YA KUTIMUA MBIO LIMEKAA KAMA BOYA! TUULIZE WENYE WAKE TOKA KANDA MAALUM TUNA MBIO HADI ZA AKIBA
HIKI NI KILANGA CHANGU NIMEJITAKIA, NIMENENG'ENEKA NIMEJIKUTA NIMETUA 'YUKREINI' HAPA NILIPO NIMESHAKUWA MATEKA NIMEZIBITIWA SIHEMI WALA SIPUMUI...BURIANI WAIF!
BABY KATA SIMU SAUTI LA MKEO LINANI-KERA!
BUZA KWA MPALANGE
NCHI ZINAZOPIGANA MARAISI WAKE WANA-NIHESHIMU SANA...NIKI-PIGA SIMU MOJA NIKISEMA ACHENI WANAACHA
WALIKUWA MADALALI WENZAKO WA NYUMBA, VYUMBA NA VIWANJA?
MUNGU ANAKUONA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIPIGIKA, JOGOO AKIWIKA UTAONA ANAKUZOMEA

# Kinachoendelea sasa Ukraine

## ■Usitishaji mapigano siku 10 waanza
## ■Watanzania ruksa kukimbilia Russia



Raia wa Ukraine wakitembea kwa miguu kwenye msururu mrefu wa magari kuufikia mpaka wa nchi hiyo na Moldova, kukimbia mashambulizi ya mabomu kutoka majeshi ya Russia juzi. **PICHA: AP**

**KYIV UKRAINE**

ZAIDI ya watu milioni tayari wameikimbia Ukraine, huku idadi kubwa wakielekea Poland, kuomba hifadhi kutokana na mashambulizi makali yanayoendelea nchini mwao.

Wakati wimbi hilo la watu wakikimbia makazi yao, Russia na Ukraine zimekubaliana kusitisha mapigano kwa muda mfupi katika miji miwili ya kusini mwa nchi ili kuwaruhusu raia kuondoka katika miji hiyo.

Russia ilisema itakuwa ni busara kuruhusu raia kuondoka katika miji ya Mariupol na Volnovakha iliyozingirwa na kukabiliwa na mapigano.

Hatua hiyo ni usitishaji mapigano wa kwanza kuafikiwa tangu Russia ilipoivamia Ukraine siku kumi zilizopita.

Huku ikiwa ni habari njema kwa raia katika Mariupol na Volnovakha wanaotaka kuondoka, ni maeneo pekee ambako makubaliano ya usitishaji huo wa mapigano wa muda mfupi yanatekelezwa.

Wakati huo huo, miji mingine inaendelea kukabiliwa na mashambulio ya mabomu.

**RUSSIA YARIDHIA KUSAIDIA WANAFUNZI WA KITANZANIA**

Ubalozi wa Tanzania mjini Stockholm Sweden pamoja na ule wa Russia zimesema kupitia njia za kidiplomasia, serikali ya Russia imeridhia wanafunzi wa Kitanzania walioko Chuo Kikuu Sumy State kutoka Ukraine kupitia mpaka wake.

Taarifa za balozi hizo, zinasema zoezi la kuwatoa wanafunzi hao kutoka Sumy hadi kwenye mpaka linaratibiwa na serikali ya Russia na tayari mipango ya utekelezaji imeanza.

"Ubalozi wa Tanzania nchini Russia utawapokea kwa taratibu nyingine za kurejea nyumbani" ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

**RAIS UKRAINE AWAFOKEA ULAYA KWA KUWAACHA**

Akiripotiwa kuzungumza kutoka katika ofisi yake katika Ikulu ya mjini Kyiv, Rais wa Ukraine Zelensky, amelaani kitendo cha viongozi wa Nato cha kukataa kufunga anga la nchi hiyo ili ndege zisiruhusiwe kupita.

Zelensky alisema "Watu wote wanaokufa wanakufa kwa sababu yenu, kuanzia leo, watakufa kwa sababu yenu. Kwa sababu ya udhaifu wenu, kwa sababu ya kutoungana."

Aliendelea kusema " Mkutano wa Nato uliofanyika ni dhaifu. Mkutano uliokanganyikiwa. Mkutano unaoonyesha kwamba sio kila mtu anayechukulia mapambano kwa ajili ya kuinusuru Ulaya kuwa lengo namba moja,".

Zelensky alizidi kulalamika"Mashirika yote ya ujasusi ya nchi za Nato yanafahamu fika kuhusu mipango ya adui. Walithibitisha kuwa Russia inataka kuendeleza mashambulizi,".

"Kwa makusudi Nato iliamua kutofunga anga juu ya Ukraine. Nchi za Nato zimebuni fikra kwamba kufunga anga za juu ya Ukraine kutakuwa ni uchokozi wa moja kwa moja wa Russia dhidi ya Nato.

Alimalizia kwa kusema "Haya ni mawazo ya kipekee ya wale ambao ni dhaifu, wasio jiamini, licha ya ukweli kwamba wanamiliki silaha nyingi zaidi ya zile tulizo nazo."

Zelensky baadaye aliuhutubia umati mkubwa wa waandamanaji wanaoendelea kuandamana katika mataifa ya Ulaya, akiwaambia waandamanaji " Iwapo Ukraine haitanusurika, Ulaya yote haitanusurika".

**MASHAMBULIZI MAKALI YAENDELEA MIJI MINGINE**

MJI wa bandari wa Mariupol ukiwa umezingirwa na kushambuliwa kwa makombora kabla ya kufikiwa kwa makubaliano, mji mkuu wa Kyiv unaendelea kulengwa na mashambulio makali.

Wakati huo huo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa litaitisha mkutano wa dharura kujadili mgogoro wa kibinadamu uliosababishwa na uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Shirika la habari la AFP lilimnukuu mwanadiplomasia mmoja ambaye alisema baada ya kikao cha Baraza la Usalama kilichopangwa kufanyika Jumatatu, wajumbe 15 wa baraza hilo watakutana kwa faragha kutafakari juu ya uwezekano wa kupitishwa rasimu ya azimio.

Mkutano huo wa faragha umependekezwa na Mexico na Ufaransa.

Nchi hizo mbili zimekuwa zikishinikiza kuwepo kwa rasimu inayotaka kusitishwa kwa mapigano nchini Ukraine na kutaka kufikishwa kwa misaada ya kibinadamu na ulinzi wa raia nchini humo.

Russia kama mwanachama wa kudumu mwenye kura ya turufu kuna uwezekano mkubwa kuwa itapinga kupitishwa azimio lolote na Baraza la Usalama, dhidi yake.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya kijeshi ya NATO Jens Stoltenberg, ametahadharisha juu ya kutokea vifo zaidi, maafa na madhara kutokana na uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

**NATO, MAREKANI ZAKATAA WAZO LA UKRAINE**

Hata hivyo, NATO na Marekani zimekataa wito wa Ukraine wa kuilinda anga ya nchi hiyo kwa kuhofia kuingia vitani na Russia Mawaziri wa nchi za NATO walitoa kauli hiyo baada ya mkutano wao wa mjini Brussels siku ya Ijumaa.

Katibu mkuu wa jumuiya hiyo, Stoltenberg alieleza kuwa NATO haimo katika mgogoro baina ya Russia na Ukraine, lakini washirika wa NATO wana wajibu wa kuzuia kuenea kwa vita.

Alisema endapo vitaenea hatari itakuwa kubwa zaidi na italeta maafa kwa binadamu.

Hata hivyo mawaziri wa nchi za NATO waliokutana mjini Brussels, nchini Ubeligiji waliahidi kuweka vikwazo zaidi dhidi ya Rais wa Urusi, Vladimir Putin.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, aliyehudhuria mkutano huo, alisema mfungamano wa kijeshi wa NATO utalinda kila sehemu ya nchi wanachama na kwamba Russia isipuuze azma hiyo ya Marekani.

Alisema kuwa mfungamano wa NATO ni wa kujihami na kwamba haitaki mzozo, lakini ikiwa itapelekewa itakuwa tayari.

Waziri huyo, alieleza NATO itaendelea kuibana Russia mpaka pale itakapobadilisha mwenendo wake.

Msaada uliotolewa kwa ajili ya Ukraine mpaka sasa ni silaha kutoka nchi za NATO na Ulaya kwa ujumla, sambamba na vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Russia.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alilaumu hatua hiyo ya NATO na kusema kuwa ni sawa na kuidhinisha mashambulizi zaidi ya Russia dhidi ya nchi yake.

Zelensky ametoa wito kwa jumuiya ya NATO kuilinda anga ya nchi yake.

Ukraine pia inataka kujiunga na NATO na kuwa mwanachama wa Umoja wa Ulaya.

Hata hivyo, Russia inapinga lengo hilo ikisema kuwa usalama wake utatishiwa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine Dmytro Kuleba, ambaye pia alihudhuria mkutano wa mjini Brussels, alizitaka nchi za NATO zichukue hatua haraka la sivyo zitachelewa.

Wakati huo huo, nchi za Umoja wa Ulaya zimesema vikwazo zaidi dhidi ya Russia vitawekwa baada ya jumuiya hiyo kuyaondoa mabenki kadhaa ya Urusi kutoka kwenye mfumo wa malipo wa kimataifa unaotumia sarafu ya dola maarufu kwa jina la SWIFT.

## MAKALA

# MFANYAKAZI WA NDANI MFANYE MWANAO



Na Magabilo Masambu

NDUGU msomaji, natumaini umeendelea kunifuatilia katika mfululizo wa makala mbalimbali ninazoandika katika safu hii. Nitumie wasaa huu kukushukuru kwa kuwa mfuasi wa maarifa haya. Naendelea kukuhakikishia kwamba hakika hujakosea kufuatilia ukurasa huu.

Leo tuzungumze kidogo kuhusu vijana na mabinti ambao tunakuwa nao katika majumba yetu, tukiwaita wafanyakazi wa ndani. Kutokana na changamoto za maisha, tumejikuta tukiwahitaji watu wa kutusaidia pamoja na kutulelea watoto.

Zamani kabla ya jamii haijawa na mawazo ya 50 kwa 50, ilionekana na kujulikana kwamba aliyepaswa kufanya kazi katika familia alikuwa baba pekee huku mama akiwa mlezi wa watoto na familia kwa ujumla. Pamoja na kwamba wamama wengi wa vijijini hali kwao ilikuwa tofauti na nafikiri bado baadhi ya maeneo imebakia hivyo, kwamba mama ndiye anayelisha familia kupitia kilimo huku bado jukumu la kulea watoto likibaki palepale. Leo mama anafanya kazi, baba anafanya kazi, jambo linalofanya ahitajike mtu mwingine wa kubaki na watoto.

Nikirejea tena, zamani ilipohitajika hivyo basi ndugu waliomba watoto wa ndugu zao ili kuishi nao kwa ajili ya kusaidia majukumu kama ya kulea watoto. Kwa sasa hali ni tofauti. Hata ukichukua mtoto wa ndugu yako leo uishi naye, atahitaji malipo. Nasema hivyo kwa sababu iwapo angechukuliwa na mwingine, basi angelipwa fedha. Siwezi kusema kwamba pengine tumependa sana fedha lakini kutokana na hali ya uchumi kubadilika, tunahitaji fedha kwa ajili ya mahitaji.

Hoja yangu leo ni kuwaeleza wale wote wenye watoto wa watu wanaowaita wafanyakazi wa ndani, kuwafanya watoto hao kuwa watoto wao kama walivyo wale wa kuwazaa. Pengine ni kwa sababu ya hali tu wanayo ya kimaisha, inawezekana vijana hao wasingekubali kutoka makwao kuja kufanya kazi za ndani kwa watu wengine.

Wale ambao tunajiweza kwa kiasi fulani, si rahisi kuwafanya watoto wetu wawe wafanyakazi wa ndani. Tunataka wasome wafanye hiki na kile ili kujitegemea baadaye.

Kwa misingi hiyo, tunaweza kubaini kwamba ni shida tu ndizo zinafanya wazazi kuruhusu watoto wao kuwa kitega uchumi walau kwa hata hicho kidogo waweze kuishi. Kama ndivyo, watoto hawa tunapokuwa nao kwenye familia zetu, lazima tutambue sababu zinazowafanya wafanye kazi majumbani mwetu, nadhani wangelipenda kuwa pamoja na familia zao kama ambavyo sisi tunakuwa na watoto wetu.

Kwanza, kauli ya kusema mfanyakazi wa ndani, mfano mtu anakuja kwako kuna watu wana tabia wanapofika kwa watu anataka kumfahamu kila mtu na uhusiano wake kwako anauliza kila anayemuona utasikia: "Huyu naye ni nani?" Hapa ndipo huwa tunakwama. Utasikia "watoto wangu ni huyu na yule huyu hapa ni mfanyakazi wangu wa ndani"

Kauli kama hizi ni za kibaguzi na hazikubaliki katika jamii ya watu wenye utu. Hivi ukimtambulisha kwamba hawa ni vijana wangu kuna shida gani? Akiuliza zaidi mwambie huyu ni mtoto wa dada au kaka yangu na umwambie kila anapoulizwa asijitambulishe kama mfanyakazi wa ndani. Hii itawafanya majirani nuksi waogope kumwingizia maneno.

Vijana hawa wanahitaji kujiona kama sehemu ya familia yako na tunatakiwa kuwajengea mtazamo huo. Jambo hili si kwa faida yake tu bali ni kwa faida yako pia. Kumfanya hivyo itamuunganisha zaidi na wanao na hata ukiwa unatoka huna wasiwasi juu ya malezi ya watoto wako maana hujiona familia moja.

Malipo unayomlipa binti au kijana wako huyo kwa hakika hayalingani na thamani ya vitu unavyomwachia. Unamlipa Sh. 40,000 kisha unamwachia watoto, nyumba na kila aina ya samani zilizoko ndani halafu unatoka kifua mbele unatamba mtaani eti unamlipa fedha, hivyo asikutanie kabisa!

Unadhani hayo malipo unayompatia yatamfanya awe na upendo kwa watoto wako? Au unafikiri yatamfanya afanye kazi zaidi? Mara nyingine unaambatanisha na matusi tena yenye kudhalilisha hata utu wake eti kwa sababu unamlipa Sh. 50,000? Akili za wapi hizi? Kitakachofanya binti huyo awapende watoto wako, afanye kazi vizuri na kwa ustadi mkubwa ni upendo wako kwake.

Kama ni mtoto na binadamu, kuna wakati anakosea kama ambavyo wanakosea watoto wako. Binti huyo akikosea, msahihishe kama ambavyo unafanya kwa wanao badala ya kumpa adhabu huku kichwani ukiwa na dhana kwamba si mtoto wako.

Baadhi ya visa vinavyoripotiwa kuhusu hao tunaowaita wafanyakazi wa ndani dhidi ya unyanyasaji wa watoto wetu ukichunguza zaidi pamoja na tabia za baadhi yao kutokuwa nzuri pengine ni kutokana na malezi. Kwa kiasi kikubwa, tatizo huwa linaanzia kwetu sisi tunaoishi nao hasa kinamama niwaseme kidogo!

Kakosa kadogo tu unapiga sana, unatukana sana, unamdhalilisha. Baada ya hayo yote, unamwachia mtoto wako mdogo unakwenda kazini. Hivi unadhani kwa akili ya kawaida tu hasira zote anamalizia kwa nani? Kama unahitaji kulinda usalama wa watoto wako, unatakiwa kuwa kama mtu anayeuza mayai akiwa amefunga kwenye 'keria' ya baiskeli na kutambua kwamba ukigongana na mwenzio tu mayai yote yanapasuka. Kwa mantiki hiyo, kuna wakati unatakiwa kuwa mpole na kuzidisha upendo kwake ili kuepusha watoto wako kutendewa vibaya.

Kuna mambo madogo tu ambayo yatamfanya binti huyo awe sehemu ya familia. Mfano unapoamua kununua nguo kwa ajili ya wanao, inagharimu nini hata yeye kumnunulia hata za kiwango cha kawaida angalau aone kwamba anathaminiwa?

Wengine wanasema kama ni pesa namlipa namnunulia wa nini? Unanunua mhindi wa kuchoma unafika nyumbani unawapa wanao pekee sababu unasema sikuwa na pesa ya kumnunulia kila mmoja! Kwa nini hicho kidogo usikigawanye angalau kila mmoja apate?

Nakubali kwamba hawa mabinti mara nyingi huwa wanaharibiwa na majirani kwa kuwajaza maneno mengi ya kipuuzi pamoja na kuwalaghai ili waache kazi kwa madai kwamba wanawatafutia sehemu nyingine. Lakini kama binti unaishi naye vizuri kila anachoambiwa atakuja kukwambia. Kikubwa mfanye akuone kama mama na baba yake kwani utu humtofautisha kati ya binadamu na mtu. Unaweza ukawa binadamu lakini usiwe mtu.

**0689157789**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Tabia Mwanjelwa, Nana Njige, Rahma Shally, wanawake waliowafungulia wenzao njia



Na Adam Fungamwango

HII ni wiki ya wanawake kote duniani ambapo kilele chake ni Machi 8 kama ambavyo imekuwa ikifanyika kila mwaka. Lengo ni kutambua mchango wa wanawake kwenye nyanja mbalimbali.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba wanawake wamekuwa mstari wa mbele si tu kuzifanya familia kuwa bora lakini kwa sasa wamekwenda mbali zaidi kwa kuleta maendeleo.

Kwa miaka ya hivi karibuni, imeonekana kuwa hata hapa nchini wanawake ndio wazalishaji mali wakubwa. Wamekuwa ndio wafanyabiashra halali na walipakodi na wamekuwa juu kwa kipato cha mtu mmoja mmoja, wakielekea kuwapiga kumbo hata wanaume.

Kikubwa hapa ni kwamba wanawake kwa sasa wamekuwa wakijishughulisha zaidi tofauti na zamani. Wala si ajabu tena kwa sasa ukaamka saa 10:00 alfajiri ukaenda kupanda daladala, ukakutana na kinamama wakienda kazini na wengine kwenye biashara zao. Wameondokana na dhana ya kwamba kinamama kazi yao ni kukaa nyumbani na kuletewa na wanaume, kitu ambacho wakati huo kilikuwa kikiwapa umaskini mkubwa na kunyanyasika.

Miaka ya nyuma ukimwona mwanamke anaendesha gari kila mmoja anashangaa ndiyo maana ilikuwa ajabu pia kuona mwanamke ni mwanamuziki. Wanawake walikuwa na vipaji vya muziki tangu zamani lakini ni wachache sana waliobahatika kuingia kwenye fani hiyo kwani hata wanaume tu walikuwa wakikatazwa na wazazi wao, sembuse mwanamke?

Ilichukuliwa kama si kazi, bali ni burudani na uhuni. Kwa sasa si hivyo muziki ni kazi. Hawa wasanii wa kike tunaowaona sasa kina Zuchu, Nandy, Vanessa Mdee na wengine wengi, msingi wao ni wanamuziki wa kike ambao walijitoa muhanga wakati huo, bila ya kujali wataonekana vipi, au kutengwa na familia, wakaamua kuingia kwenye fani hiyo.

Tofauti na wazazi wao walivyofikiri, fani hiyo iliwapatia sifa na umaarufu mkubwa, si wao tu hata wazazi na familia zao, kiasi kwamba wameendelea kukumbukwa vizazi na vizazi, tofauti na kama wasingekuwa wanamuziki.

Wanamuziki wa kike nitakao wataja hapa, wasingeandikwa, au kukumbukwa licha ya kwamba baadhi yao wamefariki kama wangeingia kwenye fani zingine, au kuolewa tu na kukaa nyumbani. Wasingejulikana na watu wengi mpaka sasa, na wangeendelea kukumbukwa na watu wachache tu, wenye nasaba nao. Ili kuonyesha kuwa muziki si uhuni, wanamuziki hao wa kike, licha ya kazi hiyo, walionewa, wakapata watoto na kuendesha familia zao kama mama.

Tabia Mwanjelwa ni mmoja wa wanawake wa mwanzo Tanzania kuvunja minyororo, kwani sauti yake ilianza kusikika miaka ya 1980 akiwa na bendi ya Maquiz Du Zaire, akiimba nyimbo kama 'Maisha ni Safari Ndefu', 'Jane', na zingine.

Baadaye alijiunga na bendi ya Orchestra King Kiki Double O chini ya mwanamuziki Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki', ingawa hakufanikiwa kurekodi. Ni mwanamuziki wa kike ambaye alikuwa akijiamini, huku baadhi wakidhani huenda si Mtanzania. Ndipo alipopata mwenzake, raia wa Zambia Rose Mwape, ambaye alirithi mikoba yake alipokwenda kwa Kiki. Mwape akiwa Maquiz aliimba nyimbo za 'Makumbele' namba mbili, na 'Nabwela miziki ya Zambia'.

Sauti hizi zilisababisha kuibuka kwa kinadada wengine wa Kitanzania, kama Emma Mkelo ambaye baadaye akawa mke wa mwanamuziki Eddy Sheggy na Nana Njige.

Hawa wote wawili waliibukia bendi ya 'Super Rainbow' chini ya Sheggy, wakaimba nyimbo nyingi kama 'Milima ya Kwetu' sehemu ya kwanza na ya pili na 'Vichekesho'.

Bendi iliposambaratika, kila mtu alichukua njia yake, Sheggy alikwenda Vijana Jazz, watoto wa kike nao wakatafuta malisho yao. Nana Njige yeye alikwenda bendi mbalimbali kama 'Legho Stars', na baadaye akaibukia Magereza Jazz na kuimba nyimbo mbalimbali, lakini wimbo uliompa sifa ni 'Ashura', ambao aliuimba kwa hisia na ustadi mkubwa.

Emma yeye alikwenda MK Beats 'wana Tukunyema mpaka chini', kabla ya kwenda Washirika Tanzania Stars na kuimba pamoja na kina Ally Choki, wimbo wa 'Ushoga Ukizidi' ambao una baadhi ya maneno ambayo anaimba Choki akijibizana na Emma 'uliyoyasema mke wangu, nimeyasikia, lakini kumbuka mwanzo wa ndoa yetu Emma, nilikueleza ushoga sipendelei, ukikaa na shoga zako, mnaacha kusukana nywele, mnaongea mambo ya umbeya.'

Kuna mwanamuziki mwingine wakike Kida Waziri ambaye alivuma na kudumu kwa kipindi kifupi, akiwa na Vijana Jazz, hasa kwenye vibao vya 'Wifi Zangu'.

Rahma Shally, yeye alionekana akiimba vizuri kwenye ngoma za asili maarufu cha JWTZ, wakati huo ngoma zote za asili ziliitwa 'Kibisa', lililotokana na kundi kama hilo lililoitwa DDC Kibisa Ngoma Troupe.

Kwa sababu kundi hilo na bendi ya Mwenge Jazz, vyote vilimilikiwa na Jeshi la Wananchi, baadhi ya wanamuziki 'walimchomoa' dada huyo kwenye kibisa na kumleta kwenye bendi. Hakuwaangusha, akaibuka na nyimbo mbalimbali kali, ukiwemo ule uliompatia umaarufu wa 'Naomba Tuheshimiane'. Sauti yake ilizifanya bendi nyingi kumnyemelea, Sambulumaa ikafanikiwa kumchukua na alikwenda kuimba wimbo uliokuwa maarufu sana 'Sitaki visa Vyako' na mwingine akiimba na Zahir Ally 'Zamaradi'. Alikwenda kujiunga na Vijana Jazz na alifanya vema kwenye wimbo wa 'Kaka Saddy.'

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-20

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwangu**
**(0716 350534)**

DAKIKA mbili za kimya zilipita, ndipo Eddy alipomwambia Mwahija. "Jumatatu naomba unipeleke mahakamani." Mwahija alionekana kushtuka "Unanitisha kuna nini tena?"

"Usihofu. Hakuna kitu kikubwa sana, ila kuna kesi."

"Umemshtaki mtu, au umeshtakiwa, mbona mpenzi hunyooshi maelezo?"

"Kesi hii na wewe unaifahamu vizuri tu. Umeshawahi kuitolea ushahidi. Ni ya yule mpwa wangu Tina Kauzeni. Rufaa imekatwa, hivyo inasikiliwa kwenye Mahakana ya Rufaa."

Macho yalimtoka Mwahija kwa mshangao. "Si iliisha, kumbe bado?"

"Upande wa mtuhumiwa haukuridhika na hukumu, kwa hiyo wameomba ipitiwe upya."

"Kama natakiwa kwenda tena kutoa ushahidi mimi sitaki. Sitoenda kabisa."

"Kwa nini?"

"Siwezi tena kumkandamiza mtuhumiwa ambaye ni ndugu wa mtu ninayempenda sana. Nitakuwa kama msaliti."

"Ambaye ni nani?" Eddy aliuliza swali la mtego. "Anajijua mwenyewe." Alijibu.

"Sikia Mwahija. Hutakiwi tena kwenda kutoa ushahidi. Wao watautumia ushahidi ule ule wa mwanzo ambao uliutoa wewe na wenzio. Kilichokuwepo wakati ule ni kwamba mpwa wangu hakuwa na wakili, wala utetezi wowote ule wenye ushahidi. Kwa sasa nimepata wakili ambaye anaweza kuisimamia, angalau apunguziwe adhabu."

"Hapo sawa, lakini kwenda tena kutoa ushahidi, katu. Nisingeweza tena. Poa mpenzi, nitakupeleka, hili lililokukuta kwa sasa ni la kwetu wote."

*******************************

Kwa sababu ilileta gumzo kubwa nchini siku ya hukumu pamoja na mijadala mitaani, vijiweni na kwenye mitandao ya kijamii, na vyombo vya habari vikawa vya kwanza kutangaza kukatwa rufani kwa kesi hiyo ya mauaji, na kupitiwa upya.




**Siku hizi ukikaa utasikia binti au kijana kaua wazazi wake, mtoto kajinyonga, mwanafunzi kajirusha ghorofani, huyu kamuua jirani yake, mwingine kamchoma kisu mpenzi wake, ili mradi kila kukicha afadhali ya jana.**

Hali hiyo ikasababisha mvuto mkubwa wa kesi hiyo, wananchi mbalimbali wakitaka kujua hatma ya kesi ya msichana Tina Kauzeni, ambaye alihukumiwa kwa kumuua bosi wake Hafidh Chilambo.

Kama ilivyo kawaida mijadala ikaanza, wakati vyombo vya habari vilipotangaza kuwa inapitiwa upya baada ya upande wa mshtakiwa kukata rufani.

Kama ilivyokuwa mwanzo tu. Wapo ambao hawakuamini kuwa msichana huyo wa miaka 18 tu anaweza kufanya kitu kikubwa kama hicho.

Wengine waliona kwenye dunia hii hakuna kinachoshindikana, hasa wakikumbuka kila kukicha kuna mlolongo wa matukio ya ajabu na ya kusikitisha.

Siku hizi ukikaa utasikia binti au kijana kaua wazazi wake, mtoto kajinyonga, mwanafunzi kajirusha ghorofani, huyu kamuua jirani yake, mwingine kamchoma kisu mpenzi wake, ili mradi kila kukicha afadhali ya jana.

Hii iliwafanya baadhi yao wasiwe na matumaini kuwa ni kweli msichana huyo, alifanya hivyo yeye mwenyewe au kuna baadhi ya watu walimtumia kwa malipo au bila yeye kujua.

Hakukucha kama siku nane zilizopita. Alfajiri ya siku hiyo ilinyesha mvua kubwa, yenye muungurumo wa radi, iliyokuwa ikitoa miale. Mvua ilionekana kama ina hasira.

Haikuzuia watu kujazana kwenye Mahakama ya Rufani kushuhudia na kufuatilia kesi hiyo iliyokuwa gumzo kubwa.

Achilia mbali wahusika, au ndugu wa pande zote mbili, lakini wanaharakati mbalimbali na haki za binadamu, mawakili mbalimbali, na taasisi mbalimbali zilionekana kuvutiwa na kesi hiyo, hivyo kutuma wawakilishi.

Florence Tinga alikuwa muda mrefu ameshafika mahakamani hapo. Yeye ndiye aliyewasilisha barua ya kukata rufani na alisimama kama wakili upande wa utetezi.

Moja kati ya watu waliowasili ni Eddy Kamal. Alishuka ndani ya gari akiwa amevaa suti yake nyeusi tii, miwani nyeusi ya jua, viatu vyeusi, ndani ya suti alivaa shati jeupe, pamoja na tai ya bluu.

Upesi, alishuka ndani ya gari na kwenda upande wa pili, akafungua mlango. Aliyeshuka ni Mwahija Chota.

Alionekana kama malkia halisi. Hakuwa kama yule aliyekwenda kutoa ushahidi mara ya kwanza juu ya mtuhumiwa Tina, jinsi alivyokwenda kununua dawa zilizotumika kumuua Chilambo.

Sasa alikuwa mtu mpya na mawazo mapya. Sasa alikuwa mikononi mwa Eddy. Alisuka rasta zilizoshuka hadi mgongoni.

Alivaa gauni lenye nakshi, ambalo lilionekana kuwa kivutio kwa wengi waliomtazama.

Kivutio zaidi kilikuwa ni jinsi Eddy alivyomfungulia mlango, akamshika mkono na kuongozana taratibu kwenda ndani ya kuta za mahakama, kana kwamba anakwenda kufunga ndoa.

Walikuwa kivutio kwa kila mtu. Hawakuonekana kama wanakwenda kusikiliza kesi ya kusikitisha. Ya msichana aliyemuua bosi wake. Kesi ya msichana ambaye tayari ameshahukumiwa kunyongwa. Kesi ambayo iwapo ushahidi upande wa utetezi usipotosheleza, basi hukumu itabaki palepale.

Wengine walidhani kuwa ni ndugu upande wa mashtaka, kwani wakati tayari kesi iko vizuri upande wao, wana uhakika kuwa utetezi hauwezi kupangua hoja nzito na ushahidi usio na shaka uliotolewa upande wa mashtaka ambao ulimtia hatiani Tina.


Kesi ya kwanza na aliyetoa hukumu alikuwa ni Jaji Paul Kilongola wa Mahakama Kuu. Rufani hii sasa ilisikilizwa na Majaji Watatu. Pius Msemwa, Edson Njau na Shaban Jeje.

Ikaanza kusomwa kwanza kwa ufupi na kutambulishwa kuwa ilikuwa ni rufani ya kesi ya mauaji, Tina Kauzeni mwenye miaka 18 akituhumiwa kumuua Hafidh Chilambo.

"Mahakama Kuu ilisikiliza kesi ile, ambayo upande wa mashtaka uliongozwa na wakili Heri Seif, na mashahidi mbalimbali, akiwemo mke wa marehemu Hellen Kisa, daktari aliyechunguza mwili wa marehemu Thomas Mtuta, pamoja na mfamasia Mwahija Chota." Jaji Jeje aliongea na kuendelea.

Pia alisikiliza upande wa utetezi, akiwemo mtuhumiwa mwenyewe Tina Kauzeni. Upande wa mashtaka ulithibitisha kwa maelezo ya mdomo na ushahidi wa vielelezo kuwa mtuhumiwa alimuua Hafidh Chilambo kwa kumuwekea aina mbili za vidonge kwenye chakula ambavyo vikichangaywa na kuwekwa idadi isiyohitajika inakuwa sumu inayoweza kumuua mtu kwa masaa mawili baada ya kunywa. Kutokana na hilo,

ITAENDELEA JUMAPILI



# MAMBO MAZURI

## KIBA AJIFARIJI KWA WATOTO WAKE

MAMBO mazuri! Inawezekana staa wa muziki wa bongo fleva, Alikiba, ametaka kuwaonyesha watu kwamba mambo yamekuwa shwari ndani ya familia yake.

Kiba jana aliweka video katika mtandao wa Snapchat, akionekana akifurahia maisha na watoto wake wawili huko Mombasa nchini Kenya.

Mwanamuziki huyo amejiunga na mkewe Amina baada ya kupita siku 14 tangu itoke taarifa ya mke wake kufungua madai ya talaka katika mahakama ya Kadhi.

Mahakama hiyo ilitoa siku 15 kwa Alikiba kufika mahakamani hapo kujibu madai mbalimbali aliyotoa Amina, ikiwamo Alikiba alikuwa hatimizi majukumu yake kama mume katika familia.

# Moni, Anjella wanataka kuikamata dunia



RAPA mkali kutoka Dodoma, Moni Centrozone, maarufu kama Malume, ameweka wazi kwamba yuko mbioni kushusha ngoma kali ambayo atamshirikisha Angella kutoka Konde gang.

Msanii huyo wa Hip hop itakuwa mara ya kwanza kutoa ngoma ambayo amefanya kolabo na mwimbaji wa kike.

Moni Centrozone ameeleza hilo kupitia post yake ya Instagram akiwa ameweka picha inayoonyesha yupo na Anjella .

"Queen Anjella Tz, Watu wa Majengo itabidi utuchapie kibwagizo kwenye mdundo mmoja wa HipHop. Itakuwa collabo yangu ya kwanza na msanii wa kike". Ameandika.

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO HAELEWEKI
KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, ambaye amekuwa akihusishwa na kazi ya ukocha Manchester United, anaripotiwa pia anafikiria kurejea katika timu yake ya zamani, Tottenham Hotspur. ***(Talksport)***

### TUCHEL HOFU TUPU
KOCHA, Thomas Tuchel anahofu Chelsea itapoteza mikataba ya walinzi - Cesar Azpilicueta, Antonio Rudiger na Andreas Christensen huku kukiwa na hali ya sintofahamu katika klabu hiyo baada ya mmiliki wake, Roman Abramovich kuiweka sokoni. ***(Sun)***

### TRAORE NJIA PANDA
BARCELONA bado hawajaamua iwapo watatoa ofa ya kuendelea kubakia na winga mwenye umri wa miaka 26, Adama Traore kwa mkataba wa kudumu mwishoni mwa msimu wakati mkataba wake na Wolves utakapokuwa umemalizika. ***(AS)***

### LEWANDOWSKI ASAKWA
MANCHESTER United wamewaomba wawakilishi wa Robert Lewandowski kuendelea kuwafahamisha kuhusu hali ya baadaye ya mshambuliaji huyo kule Bayern Munich, huku klabu ya Bavaria ikiripotiwa kujaribu kumpata mchezaji wa Borussia Dortmund Erling Braut Haaland atakayemrithi mikoba yake. ***(90min)***

### BARCA YAPEWA SHARTI
WAKALA wa Erling Haaland, Mino Raiola ameripotiwa kuiambia Barcelona watatakiwa kusaini mkataba na mteja wake mwingine, mlinzi wa kulia wa Ajax mwenye umri wa miaka 24 raia wa Morocco, Noussair Mazraoui. ***(Sport, via Express)***

### JOVIC ANUKIA DORTMUND
BORUSSIA Dortmund wanaweza kumsajili kiungo wa Real Madrid, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 24, kama mchezaji mbadala wa Erling Haaland (21), iwapo nyota huyo ataondoka msimu huu. ***(Fichajes)***

### EVERTON YASUBIRI OFA
KLABU ya Everton inasubiri ofa ya kusaini mkataba na mshambuliaji wa England mwenye umri wa miaka 24, Dominic Calvert-Lewin na straika, Richarlison mwenye miaka 24. ***(Telegraph)***

### MARTINELL: SIONDOKI ARSENAL
MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Gabriel Martinell mwenye umri wa miaka 20 amesema anataka kubakia kwa washikabunduki hao katika "maisha yake yote" na ameazimia kuisaidia kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(ESPN Brasil)***

### KLOPP APEWA MKATABA
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema hakuna kilichobadilika kuhusu mkataba wake ambao wa sasa unatarajiwa kumalizika mwaka 2024. ***(Sky Sports)***

### MARTIAL KUONDOKA SEVILLA
KLABU ya Sevilla haitajaribu kuendelea kumshikilia mshambuliaji wa Manchester United mwenye umri wa miaka 26, Anthony Martial baada ya kumalizika kwa mkataba wake mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Transfers)***

### RICE ATEMA CHECHE
KIUNGO wa kati wa West Ham mwenye umri wa miaka 23, Declan Rice, ambaye amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu na Chelsea na Manchester United, ameelezea bei ya pauni milioni 100 ambayo wagonga nyundo hao walimhusisha nayo kuwa ni "wazimu". ***(Evening Standard)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AJIPANGA UPYA KUIVAA UNITED

Ni kwa kubadilisha mfumo wake kwa ajili ya kuhakikisha wanaibuka...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola ameweka wazi anakusudia kubadili mbinu kwenye mchezo wa leo dhidi ya Manchester United ili kuzuia mashambulizi ya kushitukiza kwenye dabi ya jiji la Manchester.

Guardiola anajulikana zaidi kwa mchezo wake wa kumiliki mpira ila kwenye mchezo huo amepanga kubadilika na kutotumia mfumo wake wa kawaida na badala yake atacheza kwa mashambulizi ya kushtukiza.

Kwenye mchezo wa mwisho ambapo Manchester City walikaribishwa kwenye dimba la Old Trafford, kikosi cha Guardiola kilifanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-0, huku katika michezo mitatu ya mwisho kwa Manchester United kwenye dimba la Etihad amefanikiwa kushinda mara zote tatu.

Akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo wa leo utakaopigwa kwenye dimba la Etihad alisema; "Ni kweli tumeshinda sana kwao kuliko kwetu, lakini hakuna sababu maalum kwa hilo.

"Hiyo huwa inatokea, lakini michezo yote tulikuwa tunaangalia zaidi kushambulia na tuliadhibiwa kwa mashambulizi ya kushtukiza.

"Huo ndio uimara wao na ubora wao, Cristiano Ronaldo, Elanga, Rashford na Sancho wanapopata nafasi ya kukimbia basi huwezi kuwazuia.

"Wana kasi na wako haraka ndio maana tunakwenda kuzuia kwa dakika 90 kwa mara ya kwanza na tutawashambulia kwa kushitukiza nasi."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

MANCHESTER CITY
VERSUS
MANCHESTER UTD


1 | 1.48
X | 4.50
2 | 6.20

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI AKUTANA NA HAALAND KWA SIRI



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi ameripotiwa kukutana kwa siri na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland jijini Munich nchini Ujerumani ili kumshawishi ajiunge na klabu hiyo kwenye majira ya joto.

Barca imekuwa ikimfuatilia kwa muda mrefu mshambuliaji huyo huku klabu kubwa zingine nazo zikiwania saini ya nyota huyo, ambapo kifungu cha kuvunja mkataba wake kina thamani ya euro milioni 75.

Lakini hadi kuondoka kwake Dortmund inakadiriwa itakuwa ni euro milioni 110 ambapo hiyo itajumuisha kamisheni ya wakala wake na baba yake mzazi.

Xavi hataki kuikosa saini ya mshambuliaji huyo ambapo ripoti zinasema alifanya safari ya siri kwenda Munich Jumanne akiwamo raisi wa klabu, Joan Laporta na mshauri Jordi Cruyff ilikuwa ni kwa sababu ya kukutana na Haaland.

Baada ya gazeti la Mundo Deportivo kutoa siri hiyo, klabu haikuweza kukanusha kuwa walisafiri kwenda Ujerumani, ingawa Cruyff alisema yeye alisafiri kwenda jijini London, huku ikibaki sintofahamu kwa Xavi na rais wa klabu hiyo kuhusu safari yao.

Wiki iliyoisha kulikuwa na taarifa Laporta alifanya safari ya kwenda Monaco kuzungumza na Mino Raiola mwenyewe, kuhusu uhamisho wa beki wa kulia wa timu ya Ajax, Noussair Mazraoui na Haaland kwa pamoja.

Taarifa zaidi zinasema kwenye vikao hivyo viwili kuna uwezekano mkubwa wa Barcelona kupata saini ya Haaland, ambaye pia anawaniwa na Real Madrid.

# Tuchel ahofia kuwapoteza nyota wake

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amekubali ana wasiwasi wa kuwapoteza nyota wake baada ya mmiliki wa klabu hiyo, Roman Abramovich kuiweka sokoni.

Jumanne iliyopita Abramovich alithibitisha anaiuza klabu hiyo baada ya kuimiliki kwa miaka 19, kufuatia shinikizo baada taifa lake la Russia kuivamia Ukraine.

Wachezaji ambao mikataba yao inaisha majira ya joto kwa Tuchel hana uhakika wa kuwashawishi kubakia klabuni hapo ambao ni nahodha, Cesar Azpilicueta, Antonio Rudiger na Andreas Christensen.

Tuchel alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa jana Jumamosi dhidi ya Burnely alinukuliwa akisema, “kutoka kweye mstari wa mwisho hatuwezi kusaidia hili, lilivyo ndivyo itakavyo kuwa, huwezi jua kwenye makubaliano kuna matokeo mazuri au mabaya.

“Hatuwezi kutabiri na ningependa nisitabiri kwenye hili, kwa sababu unaweza kupoteza mwelekeo, kila mmoja yupo kwenye hali tofauti na anajisikia tofauti kutokana na kuzwa kwa klabu, natumaini matokeo yatakuwa mazuri.

“Nahisi tuna kitu tunaweza fanya bado, Chelsea ni klabu yenye nguvu na itabaki kuwa na nguvu.”

“Mmiliki wetu ameamua kuiuza klabu, lakini anaiuza klabu yenye nguvu, imara, ina umoja wa hali ya juu.”



## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# COASTAL UNION YAITAFUTIA DAWA MAALUMU KMC FC

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC, benchi la ufundi la Coastal Union limesema limetafuta 'dawa' ya kupata ushindi wa ugenini, imefahamika.

KMC FC inatarajiwa kuikaribisha Coastal Union katika mechi ya raundi ya 17 ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Coastal Union, Joseph Lazaro alisema kikosi chake kimejipanga vyema kuondoka na pointi tatu muhimu kutoka katika mchezo huo.

Lazaro alisema mechi zote za ligi hiyo ni ngumu na timu yake imejipanga kuingia kivingine kwa ajili ya kuhakikisha hawapotezi mechi hiyo.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata pointi tatu katika mchezo wetu dhidi ya KMC , tunaupa umuhimu mkubwa mchezo huo,tunajua hautakuwa rahisi kwa kila upande," alisema Lazaro.

Kocha huyo aliongeza ameshayafanyia kazi makosa ambayo aliyabaini katika mchezo uliopita ambao ulimalizika kwa sare dhidi ya Azam FC ili kuondoka na pointi zote.

Alisema msimu huu una ushindani mkubwa na wachezaji wanapaswa kupambana muda wote ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

"Nina kazi ya kuwajenga kisaikolojia wachezaji wangu ili tupate matokeo chanya na tushike nafasi za juu katika msimamo wa ligi, bado hatujafikia malengo tuliyojiwekea kwa msimu huu," Lazaro aliongeza.

Coastal Union yenye pointi 18 iko katika nafasi ya 16 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo vinara wake ni Yanga yenye pointi 42.




Kocha wa Kombaini ya Mabondia kutoka Mbagala, Ally Abdallah (katikati), akishukuru kwa niaba ya makocha wenzake ambao mabondia wao watashiriki fainali za kusaka bingwa wa Champion wa Kitaa zitakazofanyika Machi 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Ngome watarajia makubwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya ngumi za ridhaa ya Ngome, Mzonge Hassan, amesema wachezaji wake wako katika hatua ya mwisho ya maandalizi kwa ajili ya kushiriki michuano ya wazi ya Taifa itakayofanyika kuanzia Machi 20 hadi 26, mwaka huu jijini Tanga.

Mikoa yote ya Tanzania imethibitisha kushiriki mashindano hayo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mzonge alisema wamejiandaa kuhakikisha wanafanya vyema na kuipa heshima timu yao.

Mzonge alisema lengo kubwa la mashindano hayo ni kupata bingwa wa nchi na vile vile kuteua wachezaji watakaounda timu ya taifa ambayo itakwenda kushiriki michuano ya Jumuiya ya Madola.

"Asilimia kubwa ya wachezaji wangu wako kwenye kambi ya timu ya Taifa, nao watashiriki katika mashindano hayo ya wazi ili kutetea nafasi zao, endapo watapoteza katika michuano hiyo basi watajiondoa kwenye kikosi cha taifa," Mzonge alisema.

Aliongeza bado ana matumaini mabondia kutoka Ngome watafanya vizuri katika michuano hiyo kutokana na uzoefu na viwango ambao wanao.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 06/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1357 | Genoa vs Empoli | 2.47 | 3.35 | 2.80 |
| 15:00 | 1425 | St Etienne vs Metz | 1.98 | 3.24 | 3.98 |
| 15:00 | 2611 | Livingston vs Celtic | 7.70 | 4.74 | 1.36 |
| 15:30 | 4075 | Royal Antwerp vs Kfco Wilrijk | 1.66 | 3.90 | 4.64 |
| 16:00 | 1025 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.65 | 3.00 | 2.85 |
| 16:00 | 1626 | Sonderjyske vs Odense | 2.75 | 3.20 | 2.51 |
| 16:00 | 3396 | Fatih Karagumruk vs Altay | 1.95 | 3.49 | 3.64 |
| 16:15 | 1399 | FC Lugano vs FC Basel | 2.77 | 3.46 | 2.35 |
| 16:30 | 3609 | Twente vs Cambuur | 1.62 | 3.87 | 4.90 |
| 17:00 | 1029 | HNK Gorica vs Hrvatski Dragovoljac | 1.31 | 5.01 | 7.32 |
| 17:00 | 1865 | Bologna vs Torino | 2.74 | 3.24 | 2.59 |
| 17:00 | 2733 | Nantes vs Montpellier | 2.11 | 3.24 | 3.54 |
| 17:00 | 3065 | Bordeaux vs Troyes | 2.24 | 3.28 | 3.18 |
| 17:00 | 3128 | Venezia vs Sassuolo | 3.10 | 3.50 | 2.21 |
| 17:00 | 3727 | Mlada Boleslav vs MFK Karvina | 1.35 | 5.01 | 8.22 |
| 17:00 | 3939 | Fiorentina vs Verona | 2.02 | 3.59 | 3.50 |
| 17:00 | 3974 | Rennes vs Angers | 1.38 | 4.68 | 7.77 |
| 17:00 | 4743 | Watford vs Arsenal | 5.49 | 3.74 | 1.64 |
| 17:00 | 5608 | Reims vs Strasbourg | 3.29 | 3.09 | 2.28 |
| 17:30 | 2178 | Mainz vs Borussia Dortmund | 4.48 | 3.98 | 1.69 |
| 18:00 | 1785 | Anderlecht vs Oostende | 1.25 | 5.72 | 9.86 |
| 18:00 | 5080 | Aalborg vs Vejle BK | 1.55 | 4.04 | 5.52 |
| 18:15 | 2807 | Elche vs Barcelona | 6.38 | 4.41 | 1.48 |
| 18:30 | 1223 | Grasshoppers vs Servette Geneva | 2.33 | 3.45 | 2.81 |
| 18:30 | 1618 | St. Gallen vs FC Sion | 1.79 | 3.70 | 4.04 |
| 18:30 | 4606 | Moreirense vs Maritimo | 2.34 | 3.12 | 3.07 |
| 18:45 | 2474 | Ajax vs Waalwick | 1.04 | 11.79 | 28.50 |
| 18:45 | 5724 | NEC Nijmegen vs AZ Alkmaar | 5.67 | 4.11 | 1.52 |
| 19:00 | 2853 | Fenerbahce vs Trabzonspor | 2.36 | 3.20 | 2.96 |
| 19:00 | 3083 | Josko Ried vs Sturm Graz | 3.42 | 3.42 | 1.94 |
| 19:00 | 3313 | Rapid Vienna vs Austria Klagenfurt | 1.48 | 4.22 | 5.37 |
| 19:00 | 3390 | Antalyaspor vs Sivasspor | 2.45 | 3.15 | 2.86 |
| 19:00 | 5776 | Dinamo Moscow vs Spartak Moscow | 2.02 | 3.32 | 3.52 |
| 19:05 | 1225 | Lille vs Clermont Foot | 1.70 | 3.68 | 4.87 |
| 19:30 | 1083 | Manchester City vs Manchester Utd | 1.48 | 4.50 | 6.20 |
| 19:30 | 2861 | FC Koln vs Hoffenheim | 2.68 | 3.58 | 2.42 |
| 20:00 | 1525 | Lamia vs PAOK | 5.53 | 3.56 | 1.63 |
| 20:00 | 1724 | Silkeborg vs Brondby | 2.08 | 3.36 | 3.36 |
| 20:00 | 1771 | Juventus vs Spezia | 1.30 | 5.25 | 9.96 |
| 20:00 | 2119 | Atromitos vs Panathinaikos | 3.30 | 2.96 | 2.31 |
| 20:00 | 2539 | OFI Crete vs Apollon Smyrnis | 1.48 | 3.74 | 7.68 |
| 20:00 | 5543 | Aris Salonica vs Olympiakos | 3.25 | 2.71 | 2.51 |
| 20:30 | 2476 | Charleroi vs Standard Liege | 2.07 | 3.45 | 3.30 |
| 21:00 | 4331 | Pacos Ferreira vs Porto | 7.91 | 4.75 | 1.36 |
| 21:30 | 2308 | Steaua Bucuresti vs Voluntari | 1.74 | 3.43 | 4.71 |
| 22:00 | 2664 | Fortuna Sittard vs PEC Zwolle | 2.56 | 3.35 | 2.56 |
| 22:45 | 2467 | Napoli vs AC Milan | 2.15 | 3.29 | 3.44 |
| 23:00 | 3496 | KAA Gent vs Zulte Waregem | 1.24 | 5.92 | 9.86 |
| 23:00 | 5412 | Eupen vs OH Leuven | 2.76 | 3.36 | 2.41 |
| 23:00 | 5912 | Betis vs Atletico Madrid | 2.91 | 3.36 | 2.39 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Machi 6, 2022

Nipashe




Guardiola ajipanga upya kuivaa United HABARI UK 21



Beki wa Simba, Henock Inonga (jezi nyekundu), akiruka juu kuwania mpira dhidi ya wachezaji wa Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Tanzania, Botswana vitani

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 inatarajia kushuka dimbani kuwakaribisha yosso wenzao kutoka Botswana katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia (U-17), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, aliiambia gazeti hili jana wachezaji wake wana ari kubwa kuelekea mchezo huo na wamejipanga kupambana kuhakikisha wanaanza vyema kampeni hiyo.

Shime alisema wachezahi wake wote wako fiti kwa ajili ya mechi hiyo na nyota wawili waliokuwa majeruhi wamepona na wanaweza kucheza endapo watahitajika katika mfumo atakaoupanga.

Kocha huyo alisema anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu Botswana pia imejipanga kusaka nafasi hiyo ya kwenda kucheza fainali hizo za dunia zitakazochezwa baadaye mwaka huu nchini India.

"Maandalizi yetu yameenda vizuri, kila kitu kiko vizuri, hakuna mchezaji ambaye ana shida, hatujapata nafasi ya kuwaona, hizi mechi za U-17 ndio mzunguko wa kwanza unaanza, mkazo tuliokuwa nao ni mechi yenyewe, tunajua ni mashindano makubwa, wenyewe pia watakuwa na hamu ya kupambana kufanya kitu," Shime alisema.

Aliongeza kwa kuwataka wanawake kujitokeza kuisapoti timu hiyo huku akisema pia amewaandaa nyota wake kupambana ili iwasaidie katika maisha yao kupitia mchezo huo wa mpira wa miguu.

# YANGA KAZINI, SIMBA YATISHA

## ●●● Huku Minziro akiwatahadharisha vinara hao wa Ligi Kuu kwa kusema...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wakishuka ugenini kwenye Uwanja wa CCM Kirumba kuwakabili Geita Gold, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema anajivunia na kuwapongeza wachezaji wake kwa namna walivyojituma kupata matokeo mazuri.

Ni mechi muhimu kwa timu zote mbili, hasa Yanga yenye pointi 42, ikitaka kuendelea kujiimarisha kileleni baada ya Simba kuichapa Biashara United mabao 3-0 katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi usiku na kufikisha pointi 34.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema wataingia uwanjani kucheza mechi hiyo ngumu, lakini wamejiandaa kukabiliana na mazingira ya ugenini, ikiwamo changamoto ya viwanja.

"Maandalizi yanakwenda vizuri sana, mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu Geita Gold iko kwenye mfululizo wa kufanya vizuri katika mechi zake nne au tano zilizopita. Wameimarika, wamejipanga, kwa upande wetu tunajua yote hayo kwa sababu tunaanza kufuatilia wapinzani tunaocheza nao kabla ya mechi. Lengo letu lipo pale pale tunahitaji pointi tatu ambazo zitatuweka vizuri kuelekea mpango wetu wa kuchukua ubingwa," alisema Kaze, raia wa Burundi.

Naye Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Minziro, alisema Yanga wasitegemee mechi rahisi, badala yake wajiandae kupata upinzani mkali, kwa sababu ameshawanoa vijana wake jinsi ya kukabiliana na vinara hao.

Alisema anajua Yanga ipo kwenye ubora wa hali ya juu kwa sasa, lakini timu yake pia iko vizuri na imeimarika zaidi kwa siku za karibuni, ikicheza mechi tano bila kupoteza.

"Mimi kama Minziro kocha wa Kitanzania, nasema hivi, kama vijana wangu watafuata maelekezo nitakayoyatoa wakayafaye kwenye mechi hiyo, basi mtaona jinsi itakavyokuwa," Minziro alisema.

Pablo alisema tangu wamerejea nchini wakitokea Morocco katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika hawakupata muda wa kupumzika na kufanya mazoezi lakini amejivunia kuona wachezaji wake wamepambana kuhakikisha wanaondoka na ushindi katika mechi hiyo ya juzi.

Kocha huyo alisema walijua mchezo huo ungekuwa mgumu lakini wanashukuru kuona wamepata pointi tatu muhimu na mabao matatu ambayo walikuwa wanahitaji ili kuendelea na kampeni ya kutetea taji wanalolishikilia.

"Kabla ya yote nichukue nafasi hii kuwapongeza wachezaji, tumecheza katika mazingira magumu, hatukupata muda wa kupumzika wala kufanya mazoezi ya utimamu wa mwili, tumefanikiwa kupata pointi tatu," alisema na aliongeza.

"Ni pointi ni muhimu sana kwetu kwa sababu zinapunguza tofauti iliyopo na wanaoongoza ligi (Yanga), pia inaongeza hali ya kujiamini kwa wachezaji wangu kuelekea mchezo unaofuata," alisema Pablo.

Aliongeza anatambua hakuna mchezo ambao ni rahisi, licha ya kukutana na changamoto ya muda na ratiba za mechi mfululizo, lakini wataendelea kupambana katika kila mechi kusaka ushindi ikiwamo dhidi ya Dodoma Jiji FC itakayochezwa kesho.

Kuhusu hali ya beki, Shomari Kapombe ambaye hakumaliza dakika 90 baada ya kupata jeraha, anasubiri taarifa rasmi kutoka kwa daktari wa timu hiyo, Yasin Gembe baada ya kukamilisha kwa vipimo.

Naye Kocha Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati, alisema uoga wao na uzoefu wa wachezaji wa Simba ndio umewasaidia kuwapa presha nyota wake na hatimaye mabingwa hao watetezi kupata ushindi.

Vivier alisema hawakuzidiwa sehemu yoyote bali Simba walitumia uzoefu wao uliowapa wasiwasi vijana wake na kujikuta wakirusu mabao matatu ndani ya dakika 19 za kipindi cha kwanza.

"Siwezi kuwalaumu wachezaji wangu kwa sababu ya dakika za mwanzo wa mchezo na kipindi cha pili tulikosa nafasi nyingi, nina imani ni suala la bahati na sio kukosa umakini kwa wachezaji wangu," Vivier alisema.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa mabingwa watetezi, Simba kuwakaribisha Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, SL P 9